# *Ibrahimu*

Bwana akubariki.

2 Habari za jioni, marafiki. Ni majaliwa kurudi tena, usiku wa leo, kanisani ku—kuzungumza juu ya Neno, Neno la Milele la Mungu wa Milele wa Mbinguni. Ni mchovu kidogo, tulikuwa—tulikuwa na ibada mbili asubuhi ya leo kwenye Kiamshakinywa cha Ushirika wa Wafanyabiashara Wakristo, Bwana alitupa baraka kuu.

3 Jambo fulani lilitukia maishani mwangu ambalo, kamwe sitalisahau. Na kwa hiyo, ninamshukuru sana Bwana katika thibitisho la—la yale ninayojaribu kumfanyia Bwana, Bwana alilithibitisha kuwa, kwamba yalikuwa ni mapenzi Yake. Na—nanyi mnajua jinsi unavyojisikia wakati wewe, jambo fulani linapotukia namna hiyo, linakufanya ujisikie vizuri sana.

4 Sasa, nimekuwa nikiwacheleweshа kidogo, samahani kwa hilo. Na—nami nilikimbia tu, asubuhi ya leo nilifikiri nilikuwa tu nikiendelea vizuri sana, nami nikasema, "Ni saa tano kasoro dakika ishirini na tano," huku saa ilikuwa imesimamishwa kwa saa moja, Ndugu Demos alisema. Kwa hiyo nadhani hivyo ndivyo tu linavyoenda, mwajua, tunaishiwa tu na wakati, kuna mengi sana ya kusemwa, na muda mfupi sana wa kuyasema.

5 Kesho asubuhi, nafikiri saa tano ama saa tano na nusu, wakati kanisa litakapofumukana, nilikuwa ni—nije hapa, tena, kwa ajili ya ujumbe mdogo kwa kanisa, Bwana akipenda, hiyo ni baada ya mchungaji na wote kumaliza shughuli zao za asubuhi na shule ya Jumapili.

6 Na halafu kesho usiku ni, tutawaombea wagonjwa, hiyo ni iwapo watu wa kutosha watakuja kufanya hivyo. Mnaona? Hatuna budi kuwa na wa kutosha kufanyiza mstari wa maombi kama tutawaombea wagonjwa. Hapa, huyo mvulana alisema hivi majuzi alipokuwa akisambaza kadi za maombi, baada ya kufikia yapata ishirini, alisema hizo zimekwisha, kwamba hakukuwako na zingine. Asingeweza kusambaza kadi zingine, hakukuwako na wengi hivyo. Hivyo ni karibu jinsi tunavyolifikia katika kanisa dogo, mwajua, tunapokuwa na mikutano ya kanisa. Unaona, unaingia kwenye kusanyiko kubwa mno . . .

7 Halafu basi, kesho usiku, kama una wapendwa wowote wanaotaka kuombewa, sasa, tunapanga, Mungu akipenda, kuwaombea wagonjwa kesho usiku, iweni hapa saa kumi na mbili kabla ya shughuli zozote za kanisa kuanza, jitwalie kadi ya maombi, na—na uwe tayari kwa ajili ya maombi, kesho usiku. Hatujui jinsi gani, lakini tutajaribu labda kuwaombea moja kwa moja mstarini, ama chochote kile—kile Bwana atakachoongoza. Na halafu inayofuata, Jumapili ijayo usiku, tena, ni maombi

mengine kwa ajili ya wagonjwa, sisi. . .Bwana akitujalia, na akipenda.

8 Halafu Jumatano ni, Jumatano alasiri ninapaswa kuhubiri kwenye Nyumba ya Old Pisgah; Ndugu Smith, nafikiri, Smith, naamini ndilo jina lake, na ni ndugu mzuri sana. Nimefanya umishenari pamoja naye huko ng'ambo, naye ni mtu mmoja tu mzuri sana. Nami nafikiri wana namna fulani ya mkutano wa hadhara kule, kwa hiyo nilikuwa nizungumze huko Jumatano ijayo alasiri, kisha turudi hapa kwa ajili ya ibada za Jumatano jioni.

9 Halafu Jumatatu ijayo, tunajaribu kuona kama tunaweza siku moja kati ya hizo na kufika kwa Ndugu Espinosa huko San Bernardino kabla hatujaingia Bakersfield, ama, karibu na Bakersfield ambako maha-. . .Huo unaitwaje, Ndugu Gene? Visalia. Nafikiri walikuwa na ukumbi, na kuuweka kati ya Fresno na Bakersfield ili waweze kupata umati wote mbili, maana mle ndani kuna watu kutoka miji yote miwili wanaotaka kuja, nao wakauweka tu katikati pale Visalia. Kwa hiyo iweni mkiomba.

10 Kisha twende kutoka huko moja kwa moja hadi Ohio, turudi kwenye nchi yenye theluji. Nasi tutakuwa kule kwa ushirikiano na Assemblies, na watu huru, na wote, pamoja huko Ohio kwenye jumba la mikutano. Halafu basi jina la mahali hapo ni lipi, Gene? Ohio? Middletown, Ohio, ni kituo cha mpira wa vikapu.

11 Kisha tuondoke huko tushuke, ninaamini, ni Monroe, Virginia, ama mahali fulani, kule chini, ambako kuna kama inchi kumi na saba za theluji, usiku wa leo.

12 Kisha turudi kutoka huko, twende Bloomington, Illinois, juma linalofuata. Na kisha kutoka huko hadi siku kumi za mwisho, siku nane ama kumi, huko Chicago kwenye Lane Tech ambako tunaenda mara nyingi sana, ambao umedhaminiwa na Wafanyabiashara Wakristo wa Full Gospel.

13 Ndipo niko nyumbani siku moja, kisha ninaenda kaskazini mwa British Columbia, huko juu ambako theluji ina kina kirefu sana. Na kwa hiyo, niko huko juu Grande Prairie basi, nami nafikiri unaofuata ni Dawson Creek, halafu Fort Saint John, hicho ndicho kituo cha mwisho kabla hujafika Anchorage, Alaska, maili elfu moja mia tano kurudi huko msituni.

14 Halafu, Bwana akipenda, ninarudi, na kutoka huko ninaenda ng'ambo. Kisha natumaini kurudi kwenye nchi ya wenyeji hapa majira ya kupukutika mwakani, Bwana akipenda, wakati fulani mapema mwakani Oktoba, Novemba, Bwana akikawia, asipokawia, kama akinichukua kabla ya wakati huo, nitakutana nanyi Ng'ambo ya pili. Akikawia, nitakuwa pamoja nanyi, tutapanda kwenda kumwona, mnaona, na kupaa juu kumlaki hewani. Sasa, hilo huenda likatukia wakati wowote, hatujui, kamwe hatuwezi kujua.

15 Lakini, nasi ni wamishenari. Nilikuwa nikizungumza na wengine asubuhi ya leo, nao walikuwa wakizungumza kuhusu, "Unaonaje kuhusu hali ya Marekani hapa?" Ni kama tu wengine wote, wamishenari, na kadhalika, tunaamini u—uamsho uko katika nchi zingine sasa, watu huko juu.

16 Kuna karibu tu, mwajua, kuna samaki *kiasi fulani* ziwani, na wa mwisho atakaposhikwa, hakuna lingine. Mungu hataweka mwili usio wa kawaida, hatakuwa na mkono wenye vidole sita juu yake. Mnaona? Itakuwa, Mwili huo utakapokamilika, ni hayo tu. Mnaona? Haidhuru unahubiri kiasi gani, ama yale Yeye afanyayo, hapo, hakuna wengine watakaokuja.

17 Kwa hiyo, ni karibu hivyo katika nchi ya uenyeji wetu, enyi marafiki, ni saa mbaya sana tunayoishi, hamtambui. Mwulize mwinjilisti mwingine, kamwe usilichukue neno langu, ama angalia kote nchini, uone mahali unapoona umati mkubwa ukimjia Kristo. Vema, unaweza kwenda huko Bombay, India, na kupiga mbinja kwa dakika tano kumhusu Bwana, ama unene maneno manne au matano, na watu elfu tano wapo, wakilia wapate kuokoka. Hiyo ni kweli.

18 Halafu basi sisi hapa tukienda mahali mahali, na kuvuta, na kuchuja, na kuvuta, na kuchuja, haininii tu . . . Kuna jambo moja tu ambalo Wamarekani wanaweza kufanya, hilo ni kudhamini kipindi fulani huko. Wana pesa hapa, wao hawana chochote kule, wala hawawezi kukilipia, lakini bila shaka wako tayari na wanataka kusikia. Unasimama kwenye njia ya kutelemkia, makumi elfu huko nje wakipunga mikono, wakisema tu, "Laiti ungalituhubiria kwa dakika zingine tano juu ya Yesu, utamke tu maneno machache!"

19 Nilisema hivyo, naona kuna mwanamke wa Kihindi aliyeketi hapa mbele yangu, usiku wa leo. Nawe je, wewe—je, wewe unatoka India? Loo, India ya kusini. Vema, kuna nafasi nzuri sana, Bwana akipenda, Oktoba hii ijayo nitakuwa huko chini karibu na Calcutta, na—na huko Bombay, na huko juu, labda huko Thailand, nasi tunatumaini hivyo. Bwana kweli ameibariki mikutano hiyo. Usingekuwa kwenye mkutano wa Bombay nilipokuwa kule, sivyo? Uliukosa. Nadhani ulisikia habari zake. [Ndugu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Ati nini? [Ndugu huyo anasema, "Yalikuwa ni matukio yasiyo ya kawaida."] Hiyo ni kweli? Vema, hiyo ilikuwa nzuri sana. Ulikuwa ni mkutano mkubwa sana kule, hakika Mungu aliwabariki watu wenu.

20 Nami kamwe sitausahau mkutano huo usiku huo huko Bombay, maadamu ningali hai. Wao—wao, nilipokutana na Askofu wa kanisa la Kimethodisti, na wengi wa viongozi, na—nao hawakutaka niwe chini ya udhamini huo niliokuwa chini yake. Nao . . . Tayari nimechukua fedha za wanawake hawa maskini na wanaume kwenda kule, nami hakika nilikuwa

nataka kuhudumu nilipokuwa kule, kwa vyovyote vile, kama meneja aliivuruga kuhusu ra—ratiba, ama udhamini. Lakini, loo, jamani, sijawahi kuona watu wengi namna hiyo wakija mkutanoni maishani mwangu; na meya wa jiji alikuwako.

21 Na hapo ndipo yule kipofu alipofunguliwa macho akisimama pale, wakati nilipompa changamoto kila Mwislamu, na kila mmoja wao, "Njoo, ukayafungue macho yake, nami nitakuamini," mnaona. "Hebu Mungu. . ." Alikuwa mwabudu jua, sasa, macho yake yalikuwa yamepofuka, aliabudu kiumbe badala ya Muumba. Nikasema. . .

22 Nilikuwa huko chini kwenye hekalu la Jaini, mwajua, na ninii—na ninii, na Wabudha, na hao wote huko, wao, dini saba ama nane mbalimbali, na kila moja yao ikimpinga Yesu Kristo, wala haikuamini jambo hilo.

23 Kwa hiyo usiku huo, wakati changamoto hiyo kuu ilipokuja, hao wote walikuwa wameketi pale, nikasema, "Sasa, huyu hapa mtu ambaye amekuwa kipofu kwa miaka ishirini, nanyi mnafikiri ninasoma mawazo yake," mwajua, watu watakatifu, mwajua, na kadhalika, waabuduo. Ndipo nikasema, "Mnafikiri ni telepathia, kwamba ni kusoma mawazo yake, kumwambia jina lake lilikuwa nani." Hata nisingeweza kulitamka, ilinibidi kutaja tahajia zake. Mnaona? Na kwa hiyo, nikasema, "Hiyo ilikuwa ni kweli." Naye alikuwa ni mtu aliyekuwa na watoto wawili, mke wake, na mvulana mmoja aliyekuwa na miaka minane, na huyo mwingine kumi, ama kitu kama hicho.

24 Nikasema, "Sasa, mlidhani hiyo ilikuwa ni telepathia ya kiakili. Sasa, kama hiyo ni telepathia ya kiakili, basi njoni hapa, sijui lolote kuhusu telepathia, kama ndiyo, ninyi ni hodari kwake, sijui chochote kuhusu saikolojia, ninyi njoni hapa mkafungue macho yake, nami nitawafuata." Nikasema, "Dini ya Kiislamu ni kuu sana, na Kurani hii ni ya kweli," nikasema, "basi hebu kuhani wa Kiislamu aje hapa na kufungua macho yake, nami nitakuwa Mwislamu." Mnaona?

25 Nikasema, "Sasa, ninawapa changamoto, kila mmoja, katika Jina la Yesu Kristo, aje akafungue macho yake." Kamwe nisingalisema hivyo kama sikuwa nimeona ono alikuwa anaenda kufunguliwa macho, bali ninajua lilipokuwa. Hilo lilikuwa ndilo kundi nyamavu kuliko yote ulilopata kusikia, maelfu, mbona, ilinichukua saa mbili kwenye motokaa kupenya kufika kule.

26 Na kwa hiyo, mtu amesimama pale, nami nikasema, "Alisema atamtumikia Mungu atakayemfungua macho." Nikasema, "Hiyo ni changamoto kubwa kwa dini ya Kiislamu, Budha, Wajaini, Makalasinga, ama yoyote ile, hiyo hapo." Kwa hiyo, hakuna mtu aliyesogea. Nikasema, "Mbona mmenyamaza hivyo?"

27 Nikasema, "Mnajua sababu ya wao kutokuja? Ni kwa sababu hawawezi kufanya hivyo. Wala mimi siwezi, bali Mungu wa

Mbinguni amemfufua Mwanawe, Yesu Kristo, ambaye mimi ni shahidi Wake." Mnaona? Nikasema, "Niliona ono kwamba a—atafunguliwa macho." Nami nikasema, "Asipofunguliwa macho, basi mimi ni nabii wa uongo, nifukuzeni India. Kama ni . . . kama akifunguliwa macho, sasa ni wangapi wenu watampokea Kristo kama Mwokozi binafsi, na kusahau kuhusu nabii wenu wa Kiislamu, na kadhalika?" Kadiri tu unavyoona, mikono mingi, maelfu mara maelfu. Hiyo hapo, jambo ndilo hilo.

Nikamwashiria, nikamwambia mkalimani nikasema, "Usifasiri hili."

28 Nikasema, "Baba wa Mbinguni, ni—ni Mlima Karmeli tena." Nikasema, "Usingeliacha Neno Lako lishindwe, kwa sababu umenionyesha mtu ambaye alikuwa anaenda kufunguliwa macho." Nikasema, "Mungu aliyenionyesha ono la macho yake kufunguliwa, na ayafungue haya macho." Ndipo akapiga mayowe, na hapo angeweza kuona vizuri kama niwezavyo mimi, mtu mwingine yeyote, akakimbia kwa meya wa mji.

29 Ilinibidi kuondoka jukwaani, sikuwa na viatu wakati nilipotoka mle, na mifuko ya nguo zangu kuraruliwa. Nao walikuwa na misururu mikubwa mno ya watu, na—nadhani walinzi, ama chochote kile, walikuwa na hizo fimbo ndefu, mwajua, wakiwazuia namna hiyo. Nao hao watu wangekimbia wapenye chini ya miguu yao, chini ya miguu yao, wapate tu kukugusa, kutambaa juu ya migongo yao. Ilinibidi kuondoka mjini, hata, tusingeweza kutoka nje ya mji kwa sababu ya kuwa na ulinzi.

30 Basi mtu huyo ameshuhudia mbele ya gavana, ama, nanii . . . Ni nini . . . ? Rais, nafikiri ndivyo ilivyo, huko juu. Naye meya wa mji alilishuhudia, nilikuwa na jina lake, ninalo kwenye moja ya mifuko yangu sasa, nafikiri, huko chini kwenye moteli, mojawapo ya mifuko ya koti langu.

31 Nao wakanialika nirudi wapi? New Delhi? New Delhi? New Delhi, nafikiri ndiko, ambako wana uwanja mduara kule wanaoweza kuweka watu milioni moja ndani yake. Kwa hiyo, ninatumaini kurudi. Yeye angali ni Mungu. Amina. Yeye habadiliki kamwe. Saa inakuja.

32 Na kama nilivyosema asubuhi ya leo katika hotuba, kama mtu akiwahi kwenda katika nchi hizo na kuona haja ya watu hao, basi tunajionea aibu. Na kuna watu huko wanaohubiri Injili, ambao kanisa letu dogo linawasaidia wengi kadiri tuwezavyo, baadhi ya hao watu wakihubiri Injili bila viatu. Hiyo ni kweli. Wamishenari wakihubiri Injili bila viatu, labda sahani ndogo ya mchuzi wa viungo yapata mara mbili kwa juma, wakikimbia kupitia misituni, na kila mahali, wakijaribu kuhubiri Injili, nasi tukijenga majengo ya dola milioni sita, na, kana kwamba tutakuwa hapa milele, na kuhubiri Kuja kwa

Bwana kumekaribia, sielewi. Si—si—si—sitaki kuingilia hilo, tuko kwenye somo lingine, mnaona.

Sasa, jana jioni . . .

Kabla hatujalikaribia Neno, hebu na tumkaribie Mwandishi katika maombi. Na tuinamishe vichwa vyetu.

33 Baba yetu wa Mbinguni, tumekusanyika tena, usiku wa leo, katika Jina la Bwana Yesu Kristo, Mwokozi wetu mpendwa, Mwanao. Tumekusanyika katika Jina Lake, kwa sababu Yeye aliahidi ya kwamba kama wawili au watatu watakusanyika katika Jina Lake, na wangeomba chochote, kuhusu jambo moja, wanapaswa kulipokea. Sasa, Baba, sisi ni zaidi ya idadi hiyo, lakini inaonyesha tu kwamba nia Yako kukutana na Kanisa, haidhuru liko katika uchache jinsi gani, Wewe bado utakutana na watu Wako. Nasi tunaomba, usiku wa leo, ya kwamba Wewe utakuja na kutubariki.

34 Kesho, Jumapili, maelfu ya mimbara itafunguliwa kote ulimwenguni kesho, Mungu, baadhi yao tayari imefunguliwa katika nchi zingine, ni Jumapili asubuhi katika nchi zingine, tunaomba, Baba, ya kwamba utawatia mafuta wahudumu Wako, kila mahali. Watie mafuta wamishenari Wako popote walipo. Watumishi Wako wanaowaombea wagonjwa, Mungu, jalia wapakwe mafuta sana hata ishara kuu na maajabu yatafanyika, kila mahali, katika kila mtu wa kila kanisa, na kila hatua ya Ukristo.

35 Bwana, jalia uje wakati ambapo Mungu atamwaga Roho Wake hivi kwamba, kwamba wakosoaji watasukumwa nyuma, na Kanisa la Mungu aliye hai litakusanyika pamoja, kama kuku awakusanyavyo vifaranga vyake. Tujalie, Baba.

36 Tunaliombea kanisa hili ambalo limefungua milango kutuleta humu. Tunaomba kesho Wewe utambariki mchungaji, walimu wa shule ya Jumapili, kwaya, na shughuli zake zote, walei wake, mashemasi wake, wadhamini, wowote wale. Jalia asubuhi, watakapokusanyika kwa ajili ya darasa la shule ya Jumapili, jalia ishara kuu na maajabu yatimizwe, jalia Roho Mtakatifu ashuke humu jengoni, uamsho uanze, wamechinjwa chini ya nguvu za Mungu, wamelala sakafuni, kila mahali, iwe tu ni mfano kote mjini yale Mungu anayoweza kufanya wakati watu Wake wanapokusanyika pamoja na kukusanyika kuomba.

37 Nikiangalia chini, usiku wa leo, juu ya ndugu huyu wa Kihindi, na mwanamke huyu, na hawa watoto wadogo, tunashukuru sana, Bwana, ya kwamba—ya kwamba—ya kwamba wako hapa pamoja nasi, usiku wa leo, kutuonyesha tu, Bwana, ya kwamba kwa kweli, imeandikwa katika Kitabu ya kwamba Mungu hana upendeleo. Na Wewe—Wewe—Wewe unaheshimika kwa wale watakaokuabudu na kukucha Wewe katika mataifa yote. Tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hili, ya kwamba Wewe ni Baba wa ulimwengu mzima kwetu sote,

Baba wa Milele. Nasi tunaomba, Bwana, ya kwamba utatuma baraka Zako za Milele juu yetu, usiku wa leo.

38 Utusamehe dhambi zetu, kama nasi tunavyowasamehe waliotukosea, jalia kusiweko na shina moja la uchungu lililosalia mioyoni mwetu, mahali popote. Jalia Roho Mtakatifu ayasafishe maisha yetu na dhamiri yetu ili Neno hili, ambalo tunajiandaa kuleta, liweze kuja limetiwa mafuta na Roho. Jalia. . .Itahiri midomo inayonena na masikio yanayosikia, lisije likaanguka juu ya udongo wenye kina kifupi, ama juu ya miamba likachukuliwa na—na ndege wa angani, bali jalia lianguke kwenye udongo mzuri, wenye rutuba wa imani na kuzaa mara mia moja. Tujalie, Bwana. Tunayakabidhi yote Kwako, na sisi wenyewe pamoja nayo, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

39 Nimekuwa nikifurahia jumbe hizi mimi mwenyewe, kile ninachopata kutoka kwake juu ya Ibrahimu. Ni. . . Mnalifurahia? Ibrahimu. Na kuukaribia, sijui mtasema nini, maana Roho Mtakatifu huongoza tu kutoka kitu kimoja hadi kingine. Na bila shaka tunaufurahia. Sisi, jana, majuzi usiku, tulikuwa naye wakati alipoitwa na Mungu; jana usiku tulipomwona, alikuwa amejitenga na. . .utii mkamilifu. Nasi tunaona ya kwamba huwezi kubarikiwa wala Mungu hawezi kukufanyia lolote, mpaka umtii kabisa.

40 Sasa, kungekuwa na agizo dogo tu ambalo huenda nikawaambia wagonjwa: Huenda ukaja hapa, uombewe, huenda Malaika wakakuwekea mikono, wala kamwe haitakufaa chochote, mpaka kwanza uamini, na kukubali, na kukiri, kwa kuwa Yeye ni Kuhani Mkuu wa maungamo yetu. Hatuna budi kuungama kwanza, kabla Yeye hajaweza kulishuhudia mbele za Mungu, kwa kuwa Yeye ni Kuhani Mkuu, hapo kutuombea tunapokiri yale aliyotufanyia.

41 Sasa, uponyaji wa Kiungu ni nini? Je, inamaanisha, sasa, kwamba inatubidi kungojea mpaka kesho usiku tupate kuponywa? La, bwana.

“Je, inanibidi kuja kanisani?”

42 La, bwana. Mara unapomwamini Mungu na kuikubali kama mali yako binafsi, imekwisha papo hapo. Sawa.

“Niliponywa lini, Ndugu Branham? Niliokoka juma lililopita; niliokoka usiku uliopita; miaka kumi iliyopita.”

43 Uliokolewa miaka elfu moja mia tisa iliyopita wakati Yesu alipokufa kwa ajili yako pale Kalvari. Na kila baraka ya ukombozi ambayo Mungu anayo kwa ajili yako, Yesu alisema pale msalabani, “Imekwisha.” Kila kitu kimelipiwa. Ni kama tu, ulikuwa kwenye duka la rehani, ndipo Mungu akaja na kukutoa.

44 Loo, somo zuri sana katika hilo, huenda tukalifikia juma lijalo la Ruthu na Naomi, yule mkombozi wa jamaa ya karibu.

Hilo ni somo zuri. Wengi sana . . . Biblia nzima ni nzuri, na yote tu kwa sababu ni Neno la Mungu.

45 Sasa, mara unapoweza kukubali uponyaji wako ama wokovu wako, kama unatembea barabarani, kama uko, popote ulipo, mara unapolikubali, hapo ndipo unapogeuzwa.

46 Nilikuwa nikikata nyasi hapa yapata mwaka mmoja uliopita, uani mwangu na—nami nilikuwa nikijaribu, wakati mwingine ingekubidi kuvaa ovaroli yangu na kukata raundi chache, ndipo mtu fulani anaingia, ingekubidi kwenda kuwaombea, utokee mlango wa nyuma ukabadilishe nguo kisha urudi. Ndipo nikaishiwa tu na petroli, na kwa hiyo nikaanza kwenda barazani, ndipo nikaona maskini lori kuukuu likisimama mbele ya nyumba, ndipo muungwana mmoja akaja akitembea barabarani, pale, hiyo njia ndogo, naye akasema, "Ninamtafuta Ndugu Branham."

Nami nikasema, "Mimi ni Ndugu Branham."

Akaangalia hizo ovaroli, na kila kitu, akasema, "Ndivyo, bwana?"

Nikasema, "Hiyo ni kweli."

Na kwa hiyo, akasema, "Vema, Ndugu Branham, nilitaka tu kukuona kwa muda kidogo, nadhani una shughuli nyingi."

Nikasema, "Kamwe sishughuliki sana nisiweze kuzungumza juu ya Bwana."

Naye akasema, "Vema . . . "

Nikasema, "Hivi hutaingia?"

Akasema, "La, nitaketi tu hapa barazani."

47 Akasema, "Ndugu Branham," akaniambia alikotoka, akasema, "Nilizaliwa na—na kuwekwa wakfu, ama kutengwa," chochote wanachokiita, "kama Mlutheri," akasema, "Nadhani, nilipokuwa mvulana mdogo. Huo ulikuwa ndio wakati wa mwisho niliopata kwenda kanisani niujuao, isipokuwa mama yangu awe alinipeleka pasipo mimi kujua lolote."

48 Kasema, "Nimeoa," mfanyabiashara mzuri sana, kasema, "Nilikuwa na vitu vingi, ninii nyingi . . . biashara nzuri ya magari, na nilikuwa nimepata pesa nyingi sana." Kasema, "Siku moja mke wangu alishuka kwenda kwa Wapentekoste," nitalinukuu jinsi alivyofanya, kasema, "alishuka akawaendea Wapentekoste, akashikwa na Maroho." Kisha kasema, "Yeye" kasema, "alikuwa na maisha ma—mazuri."

49 Kisha kasema, "Alikuja kwangu na kujaribu kunifanya niende, na kupata hayo Maroho, nami nikasema, 'La,'" kasema, "Nikasema, 'Mpenzi, ukitaka kwenda,'" kasema, "'wewe endelea, kwa vyovyote vile.'" Kasema, "'Sasa, kumbuka, kama unabadilisha maisha yako . . . '"

50 Kasema, “Tu—tuliishi maisha ya kawaida, ya Kimarekani, karamu za kokteli, madansi, ulevi, na kadhalika.” Kisha kasema, “Nilifurahi kumwona amenyooka.” Kasema, “Alinyooka, ilimfanya mtu tofauti.” Kisha kasema, “Niliwaza, ‘Vema, kama—kama akifanya hivyo, nina—nina furaha sana kwamba anafanya hivyo.’”

51 Naye akasema, “‘Sasa, una kitabu cha hundi, wakati wowote maskini kanisa lako linapohitaji pesa zozote, jina lako linafaa tu kwenye hundi kama langu, endelea, ziandike.’” Kisha kasema, “‘Lakini kwangu mimi, mimi—mimi si wa kidini,’” Kasema, “‘Kama unataka kuwa wa kidini, endelea.’”

52 Kisha akasema kwamba, “Vema alikuwa katika maskini kanisa hilo yapata mwaka mmoja.” Kisha kasema, “Walikuwa na mkutano mkubwa huko Tennessee.” Kwa hiyo, nadhani lilikuwa ni Church of God of Prophecy, huko ndiko wao—wao wanafanyia mikutano yao mikubwa huko juu. Na kwa hiyo, akasema ya kwamba alienda kule.

53 Kisha kasema, “Nilikuwa nikiuza, motokaa, ndani, huko nje u—uwanjani,” kisha kasema, “kwa akina mama fulani,” akasema, “Ningevaa koti langu, majira ya kiangazi,” kasema, “nitoke mbele yao nipate kuuza.” Kisha kasema, “Niliporudi, ilitokea niliwazia, hivi nilimpa mwanamke huyo hiyo seti ya pili ya funguo? Nami nikaingiza mkono wangu mfukoni mwangu,” na kusema, “nilikuwa na kibandiko kidogo cha mraba mle ndani, kilikuwa na alama ya kuulizia, na nyuma yake, kilisema, ‘Utaishi wapi Milele?’” Vema, akasema, “Nikaangalia nikawazia, ‘Vema nashangaa ni nani aliyekiweka hicho mfukoni mwangu?’ Nami nikakitupa tu kwenye kikapu cha takataka.”

54 Kisha kasema, “Kitu fulani kikaniambia, ‘Lakini hilo halina budi kutatuliwa,’” kisha kasema, “Niliunyosha mkono, nikakiokota tena,” na kusema, “nikaanza kutetemeka, nami nikawazia, ‘Hiyo ni kweli. Nimepita umri wa miaka arobaini, kwa hiyo ninapaswa kuwa nikitafuta kujua mahali nitakapoitumia.’”

55 Kisha kasema—kasema, “Loo, sasa angalia hapa, unachanganyikiwa kabisa.” Kwa hiyo akakitupa chini tena, akajaribu kugeuka, akaiwasha feni, na kadhalika, ndipo kasema aliangalia nyuma yake tena, liliendelea tu kupiga kengele moyoni mwake, “Utaishi wapi Milele?” Akakichukua mara ya tatu. Naye akasema jambo hilo lilimtia wasiwasi sana hata asingeweza hata . . . akaenda nyumbani.

56 Kasema alisikia ya kwamba yule mwinjilisti maarufu, Billy Graham, alikuwa mkoa mmoja tu kutoka kwake, akifanya mkutano, akasema alihudhuria mkutano huo, akawazia angezungumza na Bw. Graham. Kisha kasema, “Bw. Graham alikuwa na ujumbe mzuri usiku huo, naye akasema, ‘Wote

wanaotaka kumpokea Yesu Kristo, simama na uinue mkono wako.'"

57 Kasema, "Nilisimama, nikainua mkono wangu." Kasema, "Waliniingiza chumbani, na kuniambia, 'Je, niliamini ya kwamba Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu?' Nami nikasema, 'Naam, ninaamini.' Nao wakaniambia, juu ya imani yangu, hilo lilinifanya Mkristo, kisha kasema, 'Yote yamekwisha sasa.'"

Akasema, "Ndugu Branham, lakini yote hayakuwa yamekwisha."

58 Naye akasema, "Nilitoka, kisha nikaenda mahali pengine, nao hao watu waliitwa Wamethodisti Huru." Kisha kasema, "Waliniambia ilinibidi kutakaswa, na kufurahi na kupaza sauti, ndipo yote yangekwisha." Kisha kasema, "Walikesha pamoja nami," akasema, "nikafurahi, nikatakaswa, na kupaza sauti, na ilikuwa . . . " Lakini kasema, "Waliniambia, 'Yote yamekwisha.' Lakini," kasema, "hayakwisha."

59 Kisha kasema, "Kisha nikamwendea ndugu maarufu Mpentekoste, ambaye huivuka nchi huku na huko," kundi mojawapo kubwa sana la Kipentekoste, na kusema, "akasema, 'Umewahi kunena kwa lugha?' 'La.' Kasema, 'Basi hujampokea Roho Mtakatifu.' Kasema, 'Basi rudi kwenye hilo hema lingine, ukampokee Roho Mtakatifu.'"

60 Kasema, "Walikuwa wazuri sana kwangu, walifanya kazi pamoja nami, na kila kitu." Kisha kasema, "Nilikaa mle ndani, kulikuwa na baadhi yao waliokaa nami hadi usiku sana." Kasema, "Hatimaye, nguvu zilinishukia, nami nikanena kwa lugha." Kisha kasema, "Nami nikatoka," kasema, "huyo mwinjilisti, nilienda kumwona kesho yake, akasema, 'Yote yamekwisha.'" Kisha kasema, "Ndugu Branham, yote hayakuwa yamekwisha."

61 Naye akasema, "Ndipo ni—nikashuka kutoka huko kwenda kwenye, kutoka huko," akasema, "Ni—nikaenda kwenye *Sauti ya Uponyaji*." Naye akasema, "Nilipofika kwenye *Sauti ya Uponyaji*," kasema, "niliingiana na hao ndugu wote kule," kisha kasema, "waliniambia ya kwamba nilikuwa nimevuka mstari wa utengano maishani mwangu, kwamba hakukuwa na nafasi kwa ajili yangu. Kasema, 'Mtu pekee anayeweza kukunyosha,' kasema, 'nenda kamwone Ndugu Branham, yeye ni nabii.'" Sasa, hilo ni kosa, lakini, "Wao walisema, 'Yeye—yeye ni nabii, ataweza kuangalia chini na kuona mahali ulipovukia mpaka, na labda utarudi nyuma na kufanya jambo fulani, kuna kitu ambacho hujafanya, ama, afadhali uende ukamwone.'"

Akasema, "Ndugu Branham, mimi hapa."

62 Nami nikasema, "Vema, Ndugu," nikasema, "Mimi si nabii." Nikasema, "Lakini Bwana huniruhusu kupambanua mambo kuwasaidia watu, karama ndogo, nyenyekevu." Nikasema,

"Lakini si—sijiiti nabii." Nikasema, "Lakini—lakini huhitaji nabii hapo, unahitaji tu kunyoshwa, hivyo tu. Huninii . . . "

63 Nikasema, "Sasa, ninataka kukuuliza jambo fulani." Nikasema, "Yale Billy Graham aliyokwambia yalikuwa ni kweli," nami nikasema, "na yale Wamethodisti waliyokwambia yalikuwa ni kweli, na yale Wapentekoste waliyokwambia yalikuwa ni kweli, lakini haikuwa kweli yote." Unaona? Nikasema, "Ilikuwa ni kweli, bali si yote."

64 Nikasema, "Ninaamini katika kumkubali Kristo kama Mwokozi binafsi, ninaamini hilo; ninaamini katika utakaso, na kusafisha maisha, na kufurahi na kupaza sauti, ninaamini hayo; ninaamini katika kunena kwa lugha, katika ubatizo wa Roho, nami ninaamini katika hayo yote," lakini nikasema, "hilo silo hasa tunalozungumzia."

Nikasema, "Nataka kukuuliza jambo fulani." Nikasema, "Sasa, kumbuka, ulisema kwa miaka arobaini ya maisha yako hukufanya lolote."

65 Akasema, "Ndugu Branham, nimeuza kila gari nililo nalo na kuwapa wahubiri na wainjilisti. Nimefanya kila kitu ninachojua kufanya, kufanya upatanisho kwa yale niliyofanya maishani mwangu."

66 Nikasema, "Hilo halikuhitajika, haikukubidi kufanya hivyo." Mnaona? Nikasema, "Mungu kamwe hakukuhitaji ufanye hivyo." Nikasema, "Huwezi kulipia njia yako ya kuingia, hilo silo wazo." Lakini nikasema, "Neema Yake inakuingiza ndani."

Akasema, "Vema, nifanye nini?"

67 Nikasema, "Hakuna kitu, hakuna kitu unachoweza kufanya." Nikasema, "Uliniambia kwa miaka arobaini ya kwanza ya maisha yako, ya kwamba hukumjali Mungu, bali uliokota kipande kidogo cha karatasi kilichosema, 'Utaishi wapi Milele?' na *Kitu fulani* kikasema, 'Hilo halina budi kutatuliwa,' usingeweza kulikwepa. Sasa, ulikuwa ukiteremka barabarani *hivi*, na mara ukaanza kurudi *huku*. Hukumjali Mungu, ukaanza kurudi ukimtafuta." Nikasema, "Papo hapo, mahali ulipogeukia, hilo hasa ndilo lililokubadilisha, papo hapo."

Akasema, "Basi nimekuwa nalo wakati wote?"

Nikasema, "Hakika."

Akasema, "Vema, Mungu asifiwe!" Mnaona?

68 Si juu ya mhemko fulani, lakini je, uliamini? Unaona? Hapo ndipo ulipo na—ulipo na . . . Unaona, sasa haidhuru ni mihemko mingapi ya utakaso . . . Kutakaswa ni mhemuko, kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu ni mhemuko, bali unapompokea Kristo kama Mwokozi wako, hilo linakugeuza. Hakuna mtu . . .

69 Yesu alisema katika Yohana Mtakatifu 5:24, wazia hilo, konzi moja na dazani mbili za mayai, mnaona, 5:24: "Yeye alisikiaye Neno Langu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna," wakati uliopo "Uzima wa Milele, wala hataingia Hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Haya basi. Unaona? Papo hapo umegeuzwa. Hiyo ni sehemu moja ya Roho Mtakatifu.

70 Utakaso ni sehemu nyingine ya Roho Mtakatifu. Ndipo unapojazwa sana Naye hata huwezi kufanya jambo lingine, kama Ndugu Rowe alivyosema, Yeye anakupa lugha nyingine basi. Na kujaribu kuninii. . . Yeye anakujaza tu, bali inahitaji Roho Mtakatifu. "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Wote alionipa Baba watakuja Kwangu." Haya basi.

71 Kwa hiyo, unapokuwa na sauti ndogo sana, inayovuma moyoni mwako ya kumjia Kristo, fanya hivyo mara moja, maana hilo ndilo jambo kuu sana lililowahi kukupata, ni kwa Mungu kukuita kwenye Karamu ya Arusi ya Mwanawe, sijui lolote lililo kubwa zaidi.

72 Sasa, tuingilie hadithi yetu, Ibrahimu, tulimwacha jana usiku baada ya yeye kupitia kwenye jaribio kuu. Naye Sara alikuwa ameamua kwamba angempa Hajiri awe mke wake, naye akamzaa mtoto na kumwita Ishmaeli. Naye Ibrahimu angali alijua ya kwamba hilo halikuwa sahihi, kwa hiyo akaenda mbele za Mungu. Ulikuwa ni mpango wa Mungu kufanya hivyo, bali Mungu alikuwa amemwahidi mtoto kwa Sara. Na sasa alikuwa na umri wa miaka mia moja, naye Sara alikuwa na tisini.

73 Basi akaenda mbele za Mungu, naye Mungu akamtokea, na kumjia katika Jina la Mwenyezi Mungu, ambalo neno la Kiebrania hapo linamaanisha "El Shaddai, Mwenyezi." Nasi tuliona, kulifafanua neno hilo, *Shad* katika Kiebrania linamaanisha, "titi." *Shaddai* linamaanisha, "Mungu mwenye matiti," Mungu mwenye matiti apate kumimina nguvu Zake Mwenyewe ndani ya watoto Wake waaminio. Wanapokuwa wagonjwa, wanapokuwa dhaifu, wakati roho imedhoofika, Yeye humimina nguvu Zake ndani yao, wanaposhika ahadi Yake yenye matiti na kuanza kunyonya, kutoka kwenye ahadi hizo, nguvu.

74 Mwenye nguvu aliye na matiti, loo, nafikiri hiyo ndiyo picha nzuri kuliko zote. Mnaona, ni faraja jinsi gani kwa mzee, mwenye umri wa miaka mia moja, angali amesimama juu ya ahadi ya Mungu! Sasa, Biblia ilisema walikuwa na umri mkubwa, uh, na umri mkubwa. Mzee, ambaye alikuwa ameshikilia ahadi ya Mungu; na kusema, "Mimi ndimi Mwenye matiti, nawe si zaidi ya mtoto anayehangaika."

75 Tumbo la uzazi la Sara lilikuwa limekauka kwa muda wa miaka arobaini, wakati wake wa kukoma hedhi umepita

kwa miaka arobaini, hamsini kabla ya hapo, labda hakuwa ameipata kwa muda, huyo hapo, mishipa yote ndani yake ilikuwa imekauka, naye alikuwa tasa. Na—naye kama—kama mwanamume, alikuwa ni kama mfu, hakuwa *mwanamume* tena kwa njia hiyo. Naye huyo hapo mzee, na mkewe mkongwe sana, naye Mungu akasema, "Lakini Mimi ni Mama," amina, "Mimi ni Mama, chukua tu, endelea kushikilia ahadi Yangu na uendelee kunyonya, ninaweza kukufanyia jambo fulani." Loo, napenda hilo.

76 Na kumwonyesha yale atakayofanya, Yeye alibadilisha jina lake katika mlango wa 17, kisha akabadilisha jina la Sara. Hiyo ni kweli. Angalieni majina hayo, yanamaanisha jambo fulani. Kwa nini akabadilisha jina la Yakobo likawa *Israeli*? Kwa nini akabadilisha jina la Sauli likawa *Paulo*? Kwa nini akafanya mambo hayo yote? Baada ya Yeye kushinda na kuingia Utukufuni, Yeye alisema ya kwamba Jina Lake lilibadilishwa. Katika Ufunuo, imetolewa ahadi kwa wale wanaoshinda, Yeye angewajulisha Jina Lake jipya. Hiyo ni kweli. Kila waliposhinda, walipewa jina jipya.

77 Ibrahimu, hatimaye aliposhinda, aliondolewa katika jina la Abramu, kasema, "Wewe hutaitwa *Abramu* tena, bali utaitwa *Ibrahimu*." Akampa sehemu ya Jina Lake, akabandika Jina Lake kwalo, *Elohimu*. H-i-m-u na h-a-m-u, Elohimu. Kwa maneno mengine, "Mimi ni Baba wa vitu vyote," mnaona, "nami ninakufanya baba wa mataifa, kwa hiyo nimebadilisha, na kukupa sehemu ya Jina Langu, *baba wa mataifa*, h-a-m-u." Mnaona? Elohimu, Ibrahimu. Hiyo ni sentensi nzuri, hivi uliwahi kuwazia hilo? Mwinjilisti mashuhuri siku hizi, jina lake Graham, G-r-a-h-a-m, Billy Graham, wazia hilo. Jinsi ambavyo Mungu katika rehema Zake, jinsi anavyojua kimbele, na mambo anayofanya!

78 Sasa, angalieni alilofanya pale, alimbadilisha *Sarai* akawa *Sara*. Jina la Sarai, *Sarai*, kuwa *Sara*. Angalieni hapo, *Sara* maana yake ni, "binti mfalme." Naye alikuwa, "baba wa mataifa." Loo, hilo si ni zuri? Kwa huyo mwanamume mzee na mwanamke mkongwe, mwenye umri wa miaka mia moja sasa, hiyo ahadi inakaribia kutimia.

79 Sasa, tunaona ya kwamba baada ya jambo hili, Ibrahimu alikuwa. . .alitengwa, akatoka na kumleta ndugu yake, Lutu, akamrudisha ndani. Basi alipofanya hivyo, kumrudisha kutoka kwa adui ambaye angalimwua, akamrudisha, akiwazia, labda, pengine angetoka nje sasa, na kujitenga na mambo yote ya ulimwengu. Badala yake, alishuka moja kwa moja akaingia Sodoma; kama nguruwe kwenye kugaagaa kwake, na mbwa kwenye matapiko yake, wanarudi moja kwa moja tena.

80 Hapo ndipo nimekuwa nikikemea hilo *sana*. Ninii. . . pamoja na. . .Haijalishi ninalikemea kiasi gani, litatendeka,

kwa vyovyote vile. Lakini kwenye Siku ya Hukumu wakati urekodishaji huu uliofanywa Mbinguni, kumbukeni, utajibu dhidi yenu. Hiyo ni kweli.

81 Kanisa la Kipentekoste, likiingia baridi na kuwa la kawaida, likirudi moja kwa moja kwenye kilindi chake cha madhehebu, na, "Maadamu sisi ni wafuasi wa kanisa, hilo tu ndilo linalohitajika."

82 Huna budi kuzaliwa mara ya pili, huna budi kuwa na Roho, huna budi kuwa na matendo, ishara na maajabu, na kadhalika, kama Mungu alivyoahidi, na hapo ndipo ninapoona kanisa likipoa.

83 Haidhuru ninahubiri kiasi gani dhidi yake, ningeweza kusimama na kusema wanawake wasivae kaptura, wanawake wasikate nywele zao, watafanya hivyo, kwa vyovyote vile. Ninaweza kusema makanisa ya Kipentekoste yanaweka pesa katika vitu vikubwa mno, na kuingiza mtindo, na kuunda dhehebu, na kuyakatilia mbali mengine yote, kama tu vile makanisa mengine yalivyofanya, yaliyoanguka kabla yao, watafanya hivyo, kwa vyovyote vile, Mungu alisema wangefanya hivyo. Lakini kile ninachojaribu kufanya, ni kuwashtua, na kuwanyakua, na kuwavuta kutoka humo.

84 Leo mkutanoni, nilipokuwa nikihubiri, Roho Mtakatifu alishuka juu ya mvulana mdogo, naye akaja pale, na kunena katika lugha ya Kifaransa, bila kujua hata neno moja la Kifaransa. Naye mtu aliyesimama pale, hatukujua tafsiri yake, wawili wao, mmoja amekuwa mkalimani wa UN, akanena, naye Roho Mtakatifu akanena na kuthibitisha ya kwamba Roho Mtakatifu alikuwa amenituma kwenda kufanya kazi hii, na kudumu mwaminifu kwake, na kudumu nayo haijalishi ni nini. Watakuwa wakiisoma moja. . . Mnaona, ikionyesha moja kwa moja miongoni mwa Wapentekoste. Naam, bwana.

85 Ndugu, jihadhari, kimbilia Mwambani, nenda kwenye Nyumba ya makimbilio. "Jina la Bwana ni Ngome imara, wenye haki huikimbilia, wakawa salama." Zile kuta kuu za Babeli zinaporomoka.

86 Kama vile huko India wakati mlipokuwa na tetemeko la ardhi kule, nadhani, ule mwaka tu nilioingia, ni kama miaka sita iliyopita. Nilichukua lile gazeti, gazeti la Kiingereza, lilisema, "Nadhani te—tetemeko la ardhi limekwisha." Huko India, hawana nyua nzuri, na kadhalika, kama mlivyo nazo hapa, wanaokota mawe na kutengeneza nyua. Wanyama wanasimama pale kwenye kivuli cha jioni, maskini ndege wanaingia mle na kujenga viota vyao.

87 Siku moja waliwaona maskini hao ndege wote wakiruka, wakiondoka, na ng'ombe wote wasingeingia ndani, kusimama kuzunguka hizo kuta, na kadhalika, walitoka wakaenda katikati ya uwanja na kusimama wakiegemeana kwenye jua.

Walishangaa shida ilikuwa ni nini. Ndipo tetemeko kubwa la ardhi likapatikisa mahali hapo, likazitikisa kuta zikaporomoka.

88 Ilikuwaje? Maskini hao ndege wote, kama wangalikuwa kwenye mabanda hayo madogo pale, wangeuawa. Wanyama wangalikuwa wamesimama chini ya nyua hizo kubwa za miamba na kuta, zingewaangukia na kuwaua. Ilikuwa ni kitu gani? Mungu, kwa silika, akiwajulisha tetemeko la ardhi lilikuwa linakuja, walikimbia wapate usalama. Kama Mungu. . . Mungu yule yule aliyewaita ndani ya safina, aliyekuwa amewaita watoke ukutani, Yeye ni Mungu yeye yule.

89 Vema basi, kama Mungu anaweza kumtumia ng'ombe, na farasi, na kondoo, na ndege kwa silika kuikimbia ghadhabu ijayo, afadhali uondoke kwenye kuta hizi kubwa za Babeli na kumkimbilia Yesu Kristo, maana zitaporomoka na kuanguka moja ya siku hizi. Mnakumbuka, kulikuwa na Jiwe lililochongwa mlimani bila kazi ya mikono, likaja likibingirika likaingia Babeli, na kubomoa popote lilipoenda. Nazo falme za ulimwengu huu zitaanguka bila shaka. Kila ufalme wa kujitengenezea hauna budi kuzama, ili Ufalme wa Mungu uweze kuwa na haki ya kuingia.

90 Kila shirika la kujibunia litaanguka na kuporomoka hata mavumbini, kusudi nguvu za Roho Mtakatifu zipate kulitwaa Kanisa na kulinyakua hadi Mahali pale juu. Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Wao. . . Kila kitu kimetumikia kusudi lake, bali tuko kwenye huo wakati, ndugu, wakati Mungu anapowaita watu Wake watoke. Lile Jiwe lililochongwa mlimani bila kazi ya mikono linabingirika, likiipondaponda Babeli, likisonga mbele moja kwa moja. Ondoka kwenye hizo kuta kubwa, rafiki, ingia ndani ya Yesu Kristo, hapo ndipo Mahali pekee pa usalama ama kimbilio nipajuapo.

91 Tunaona hapo ya kwamba Ibrahimu, alipoona kile Mungu alichomtaka afanye, Yeye alimbariki na kubadilisha jina lake, na kubadilisha jina la Sara, akawapa ahadi ya—ya—ya hakika ya kwamba jambo hili litatukia, ndipo tunamwona, ninaamini ni katika mlango wa 18, tunamwona ameketi huko nje kondeni, mahali fulani jangwani, njia ngumu.

92 Jamani! Loo, sijui ni kwa nini hilo linaendelea kububujika ndani yangu. Mimi. . . Samahani, la, msinisamehe, sasa, hilo—hilo lingekuwa ni kosa. Ni kwa nini, ndugu? Nilisimama, hapa si muda mrefu uliopita, miongoni mwa kundi kubwa la watu wazuri, Wapentekoste, nami nikasema, "Mnatoa shuhuda mbaya. Daima mnazungumza kuhusu jinsi Mungu anavyowabariki, mna vitu vingapi vikubwa, mnaweza kumiliki Kadilaki ngapi, na yote namna hiyo, hiyo ni tofauti sana, na vile Pentekoste ya kwanza ilivyokuwa, waliuza kila kitu walichokuwa nacho, na kuwapa maskini, nao wakaenda

wakihubiri Injili. Kuna kasoro, mahali fulani." Hiyo ni kweli kabisa.

93 Kulikuwako na jamaa aliyesimama, akasema, "Na Ndugu Branham, hilo ndilo kosa kubwa sana walilowahi kufanya hao watu." Tulikuwa huko Jamaika. Kama mtu yeyote yuko hapa, Ndugu Bonamore, nadhani unakumbuka, sijui kama Ndugu... naam, alikuwa pamoja nami, akiketi huko nje usiku huo.

94 Nikasema, "Unataka kuniambia ya kwamba unafikiri kwamba Mungu hukosea? Mungu hakosei, mtu anayeongozwa na Mungu. Waliongozwa na Mungu kufanya hivyo."

Akasema, "Ndipo wakati mateso yalipokuja, hawakuwa na makazi yoyote ya kwenda, nadhani unafikiri hilo lilikuwa ni kosa."

95 Nikasema, "Jionee aibu! Hujui zaidi, umekuwa katika Pentekoste muda wote ambao umekuwa, humjui Mungu zaidi ya hapo. Hivyo ndivyo hasa ilivyombidi Mungu kufanya, hawakuwa na kitu cha kurudia, wakaenda kila mahali, wakiusambaza Ujumbe kote nchini. Mungu anajua analofanya."

96 Akaacha waongozwe, hakika. Mungu hafanyi makosa yoyote, mimi na wewe ndio tunaokosea, Mungu hakosei. Unapojisikia kuongozwa na Roho, songa mbele, songa mbele, endelea tu kusonga mbele.

97 Hapa Ibrahimu, hakuwa huko chini Sodoma, akiona ni kiasi gani angeweza kupata, alikuwa huko juu kondeni katika kumtii Mungu. Labda Sara hakuwa na nguo mpya ambazo Bibi Lutu alikuwa nazo, hakuendana na mitindo yote, hata hivyo walisema hapakuwapo na mwanamke mrembo nchini kama alivyokuwa. Alikuwa ni mama, naye pia alimpenda mumewe sana hata hakuzibana nguo zake na kutoka nje mtaani, na kufanya yasiyofaa jinsi Bibi Lutu wa kisasa afanyavyo, na mambo kama hayo, alimwita mumewe *bwana*, nayo Biblia ilisema, "ambaye ninyi ni binti zake, maadamu mnalitii Neno." Hiyo ni kweli.

98 Huyo hapo. Nasi tunawaona huko nje, nyakati ni mbaya, mifugo inapungua, kila kitu kilionekana kuwa, bali Ibrahimu alikuwa akidumu katika ile ahadi. Amina.

99 Hapo ndipo tunapofanyia makosa yetu, ndugu. Si madhehebu yetu yanayokosea, ni sisi katika madhehebu tunaokosea. Mnaona? Ni sawa maadamu wewe, kama utadumu katika ahadi, lakini unapoingia katika mambo haya unaanza kuwa mgumu, unataka kutenda kama walimwengu wengine. Hiyo ndiyo sababu Mungu anayaondokea moja kwa moja.

100 Ninamtazama usoni mmoja wa wanahistoria mashuhuri sana walioko Marekani, nami nitakwambia, Ndugu Paul Boyd, uliyeketi papo *hapo*, nami nitakwambia jambo moja, hebu nionyeshe chembe moja ya historia ambapo kanisa lilipata kuingia katika dhehebu, kama halikuanguka, wala halitainuka

tena. Litafute. Kamwe halikuwahi, kamwe halitakuwa, si mapenzi ya Mungu. Tutalifikia hilo juma lijalo.

101 Angalieni, lakini sasa, tunapoendelea na Ibrahimu, Ibrahimu alikaa nchini, alikaa papo hapo, mahali ambapo Mungu alimwambia. Na maadamu alikaa kule, Mungu alikuwa pamoja naye, alipoondoka nchini, laana ikamjia. Mara unapoondoka kwenye ahadi ya Mungu, basi jitayarishe tu kupata matatizo. Hiyo ni kweli kabisa.

102 Sasa, tunaona ya kwamba siku moja alikuwa ameketi pale nje. Hebu tuliigize kidogo kusudi jamaa hawa wadogo hapa waweze kulipata. Sasa, ninamwona Ibrahimu ameketi kwenye mlango wa hema asubuhi moja, kulikuwa na mwaloni mkubwa mbele ya makazi yake pale. Wanadai mwaloni huo ungali unasimama, wameuhifadhi, wanasema, vema, hapo ndipo alikuwa amepiga hema lake, huko nje jangwani.

103 Lutu alikuwa huko chini, jamani, nami nadhani kama walikuwa na kitu kama hicho, angekuwa na msokoto mkubwa, na meya wa jiji, mwajua. Naye Bibi Lutu, na binti zake, na hao wote wakienda kwenye maonyesho yote ya mitindo, wakiangalia televisheni, na—na kuiga mi—mi—mitindo ya siku hizo. Lakini Sara alisimama mkweli, Ibrahimu alisimama mkweli, walidumu pamoja na Mungu, wakakaa huko nje.

104 Sasa, ilikuwaje? Siku moja wakati Ibrahimu alipokuwa ameketi pale, yapata saa tano mchana, ninawazia, aliangalia, wakija kupitia pale, na hawa hapa watu watatu wakaja huku nguo zao zimejaa vumbi, wakitembea.

105 Mnajua kuna jambo fulani kulihusu, unaweza kupita moja kwa moja karibu na baraka za Mungu wala usijue, kama hujaomba vya kutosha. Ninawazia juu ya jambo hilo, kuomba vya kutosha.

106 Kulikuwako na maskini mwanamke wa Kiairishi aliyekuja kutoka Ayalandi, si muda mrefu uliopita, nao wakasema alikuwa kwenye meli naye alikuwa. . . Yapata, loo, yapata wakati walipokuwa wakifika huko New York tufani kubwa ilipita kasi baharini, nayo meli ilikuwa tu ikituma kilio cha msaada SOS, nayo ilikuwa tu ikipiga mbizi mahali mahali.

107 Bendi zilikuwa zikicheza, walikuwa wakicheza roki yote waliyoweza na yote namna hiyo. Ndipo wakaanza, bendi ikaanza kuomba, nahodha akasema, “Kila mtu aombe, kila mtu aombe, jinsi unavyofanya kanisani mwako.” Nao, bendi zikaanza kucheza *Karibu Nawe Zaidi, Mungu Wangu*. Nao wote wakaanza kupiga nduru.

Maskini mwanamke wa Kiairishi akaanza kutembea huku na huku sakafuni.

108 Naye nahodha akasema, “Laiti tungaliweza tu kushikilia dhoruba hii kwa dakika thelathini, tutaingia bandarini, tutie

nanga." Kasema, "Lakini kama hatuwezi kuishikilia kwa dakika thelathini," kasema, "tutakuwa chini ya bahari."

Maskini mwanamke huyo wa Kiairishi akasema, "Mungu atukuzwe! Haleluya!"

Kwa hiyo nahodha akakaribia, akasema, "Mama, ulielewa niliyosema?" Akasema . . .

Akasema, "Nilikuelewa dhahiri, bwana."

Akasema, "Nilisema mnamo dakika thelathini tangu sasa huenda tukawa chini ya bahari, kama hatuwezi kushikilia dakika thelathini katika dhoruba hii."

Kasema, "Nilielewa ulichomaanisha." Kasema, "Haleluya! Mungu asifiwe!"

Kasema, "Kwa nini usiombe?"

Akasema, "Nimeomba vya kutosha tayari, hainibidi kuomba tena." Kasema, "Kwanza kabisa niliomba vya kutosha."

Vema, kasema, "Kwa nini ukasema *haleluya* namna hiyo, na ukijua ya kwamba huenda ukawa chini ya bahari?"

109 Akasema, "Bwana, niko njiani kutoka Ayalandi kumwona binti yangu anayeishi New York." Akasema, "Nina binti Utukufuni na mmoja huko New York, kama tukizama, nitamwona huyo Huko juu, kama tukitua, nitamwona huyo huko, nitamwona mmoja wao katika dakika thelathini."

110 Hiyo ni kweli. Kuomba vya kutosha! Amina. Hiyo ndiyo njia ya kukaa, umeomba vya kutosha, kuwa tayari kwa ajili yake. Alikuwa anaenda kukutana na mmoja wao katika dakika thelathini. Alijua ama . . . Haikuleta tofauti yoyote kwake, Huko juu, ama huku chini, haikuninii . . . anaenda kumwona mmoja wao katika dakika thelathini. Sasa, hilo ni zuri, hilo ni sawa. Hivyo ndivyo Kanisa linavyopaswa kuwa wakati wote, limeomba vya kutosha.

111 Ibrahimu aliomba vya kutosha, ameketi huko nje. Lutu hakujua, labda, huko chini, kile kilichokuwa kikiendelea huko nje jangwani. Lakini Ibrahimu alipoangalia, kulikuwa na jambo fulani kuhusu Mtu huyo anayetembea pale mbele ambalo alitambua kwamba kidogo lilionekana la kigeni. Loo, jamani! Mtu aliyeonekana wa kigeni, akatoka mbio, na kama mkiangalia, jambo la kwanza kabisa alilosema, "Jamani," si "Bwana *Zangu*." Hakika sikubaliani na yule ndugu Myahudi aliyetoa tamshi hilo hivi majuzi usiku huko Shreveport. Si "Bwana *Zangu*," bali, "Bwana *Wangu*." B-w-a-n-a, mmoja. "Jamani," herufi kubwa B-w-a-n-a, "karibu ndani."

112 Sasa, yupo mmoja wenu anayemwona mfasiri hapo? Huyo alikuwa ni Elohimu, Ibrahimu alimwita. Akamwingiza ndani, kasema, "Waweza kuingia, uketi chini? Nitakuletea maji kidogo, nitaiosha miguu Yako. Nichukue kipande cha mkate." Kisha

akasema, “Basi Wewe, ridhisha shauku Yako—Yako, ndipo unaweza kwenda popote unapoenda.”

Ninaweza tu kuwazia akiingia kisiri, na kusema, “Sara, Sara, *shh*! Mtu fulani yuko huko nje, andaa unga, upesi sana, ama, unga wa mahindi.”

113 Basi ni wangapi wamewahi kuona kichujio? Kuna wanawake wowote hapa. . .? Vema, mnatoka sehemu gani ya Kentucky? Nilizoea kumwona Mama na kichujio hicho cha kale, akienda kwenye pipa la unga, naye alikuwa na kitu kidogo cha duara, kama kreti ya jibini na waya wa skrini chini yake, na kukitumbukiza namna *hii*, pia alikuwa na kabari kuukuu mle ndani, angezisugua taa kabisa wakati huo unga wa kale ungelowa maji. Je, mmewahi kuona hilo likifanywa?

114 Mwajua, hivi majuzi, nilimnunulia mke wangu kinu cha kahawa hapa chini, kimoja cha hivyo unavyosaga mwenyewe. Mbona, sijasaga moja tangu nilipokuwa mvulana mdogo. Ni. . . Kilikuwa ni changu, na kusafisha dohani ya taa, mwajua, unaingia mle ndani pamoja na maskini mwezi na bundi kwenye taa ya bomba. Mnavikumbuka? Ilibidi kuingiza mikono yangu mle chini na kuisafisha.

115 Nami ninamwona Ibrahimu akikimbia, na kusema, “Aisee, chukua, kanda u—u—unga kidogo sasa hivi, na uutayarishe, uoke keki kwenye makaa.” Akatoka akaenda na kumwagiza mtumishi amchukue ndama na kumchinja, kisha atoke akawalishe Watu hawa.

116 Sasa, wanajifanya kana kwamba walikuwa ni wageni, walikuwa wametoka Nchi nyingine, nao walikuwa tu wakipita. Na kwa hiyo, ninawazia tu, labda kwamba Ibrahimu alichukua maskini kiwinga inzi na kutoka huko nje, mwajua, inambidi kutoka nje na kuwawinga. . .

117 Ni wangapi wanaojua kiwinga nzi ni nini? Sasa najua kuna Wakentaki hapa, sasa. Naam, bwana. Ninakumbuka wakati watu wangekuja, tungewaweka huko nje, na kuchukua maskini hicho kiwinga nzi, nami ilinibidi kusimama, maskini mkono wangu karibu ungevunjika, namna *hiyo*, nikiwawinga tu nzi, wakati Mama alipokuwa akipika. Halafu, baadaye, unasimama karibu na jiko hilo na kupangusa jasho, na, kwa kiwinga nzi hicho, mwajua, ukikifanya *hivi*, ili kwamba nzi wasije wakazunguka mahali sisi *tsk*. Tulilelewa maskini.

118 Na kwa hiyo, tulichukua siagi na malai, na kuviweka kwenye nyumba ya maziwa, ama, si nyumba ya maziwa, bali maskini mahali padogo, kule chini kwenye kijito, na kuufunika kabisa, huo mtungi, mwajua, na maziwa yanafikia. . .malai yanakuwa na kina *hicho*. Niliingia humo kisiri mara nyingi, nikachota kikombe chake, wakati alipokuwa akijaribu kuyahifadhi. Loo, nini, yalikuwa mazuri!

119 Sasa, tunaona ya kwamba Ibrahimu alipeleka chakula hiki huko nje na kukiweka mbele ya watu hawa, nao wakala. Sasa, Ibrahimu alikuwa na shauku ya kujua safari yao ilikuwa ni nini, kwa sababu alijua ya kwamba Mmoja wao pale, Yule mkuu, alikuwa ni Mungu. Alijua Huyo alikuwa ni Mungu, alimwita *Elohimu*. Kwa hiyo sasa, iliwakilisha nini?

120 Tunaona ya kwamba wawili wao walisimama na kushuka kwenda Sodoma, walikuwa wakishuka kwenda kule kuhubiri, na kuwaita wale ambao wangeitwa watoke. Nasi tunaona ya kwamba alipofika kule chini na kuanza kuhubiri, kwamba hawakufanya miujiza mingi, waliwapofusha tu. Hiyo ilikuwa . . . Kuhubiri Injili hupofusha.

121 Lakini kulikuwako, sasa kumbukeni, kuna matabaka matatu, daima. Kwenye ile Hukumu tunaona ya kwamba Bibi-arusi anarudi pamoja na Kristo; katika Danieli, elfu kumi mara elfu kumi walikuja pamoja na yule Mzee wa siku, Hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunguliwa; na Kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho kilikuwa ni Kitabu cha Uzima. Mnaona, yule mwanamwali aliyelala alikuja kwa ajili ya Hukumu. Ndipo kitabu cha wasio haki kikafunguliwa, Naye akawatenganisha kondoo na mbuzi. Lakini Kanisa lililonyakuliwa likarudi pamoja Naye.

122 Yesu anakuja mara tatu: Alikuja kwanza kumkomboa Bibi-arusi Wake, anakuja mara ya pili kumnyakua, anakuja mara ya tatu pamoja Naye; kumkomboa Bibi-arusi Wake, kumpokea Bibi-arusi Wake, na kumrudisha Yeye pamoja na Bibi-arusi Wake kama Mfalme na Malkia juu ya dunia, akaketi kwenye kiti cha enzi cha baba Yake, Daudi.

123 Na sasa, tunajua kuna matabaka matatu ya watu wakati wote. Tunaona jambo hilo siku hizi, kumekuwako na Walutheri, Wamethodisti, Wapentekoste. Kuna mwenye dhambi, mwovu, mwanamwali aliyelala, na mwanamwali wa kweli, daima. Sasa, tunaona kulikuwa na Wasodoma; kulikuwako na Lutu, lile kanisa vuguvugu; na huyu hapa Ibrahimu, alikuwa amejitenga nao, nao waliishi mbalimbali. Sasa, neno lenyewe *kanisa* linamaanisha "utengano."

124 Israeli walikuwa watu wa Mungu mpaka walipofika nyikani, kisha wakiisha kuitwa watoke, wakawa ni Kanisa la Mungu basi. *Kanisa* linamaanisha "walioitwa watoke, waliowekwa kando." Naye Ibrahimu alikuwa ni Kanisa teule; Lutu alikuwa yule bikira aliyelala, ama kanisa la kawaida; halafu kulikuwako na mwenye dhambi, Wasodoma.

125 Sasa angalieni, Wasodoma, na watu wa kawaida huko chini, Lutu katika hali yake ya kawaida, sasa, alikuwa ni mtu mzuri, hapana shaka, Hiyo ilisema, "Dhambi za huo mji ziliitesa nafsi yake yenye haki." Lakini kulikuwako na Kanisa teule, lililoitwa, lililochaguliwa tangu zamani na Mungu, Ibrahimu, aliyeitwa

wakati alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano, akapewa ahadi, kusudi hilo jaribio liseme litakuwa la hakika. Ngojeni mpaka tutakapofika mbele kidogo hapa, ambapo Yeye alilifanya la hakika kabisa.

126 Vema. Akamwambia kuhusu mtoto atakayempata, wala Ibrahimu hakusita katika ahadi ya Mungu. Haidhuru ni dola ngapi za ziada zilizowekwa hapa chini, na jinsi angeweza kuwa tajiri huko Sodoma, na yale aliyoweza kufanya, alidumu pamoja na Mungu, akatimiza ahadi, hilo ni Kanisa teule. Kuna baadhi yao katika Wamethodisti, wengine katika Wabaptisti, wengine katika Wapentekoste, Kanisa teule litaitwa litoke katika makundi yote. Hiyo ni kweli. Hilo ndilo linaloisikia ile Sauti.

127 Wakati Yesu alipokuja, Bwana Yesu Kristo, kwa nini hawakumtambua? Hawatambui jambo hilo mpaka limechelewa kupita kiasi.

128 Hawakujua kamwe Elisha alikuwa ni nabii wa Mungu. Mbona, waliwatuma watoto wao kumtania, wakamwita mwenye upara, kwa sababu alipata upara alipokuwa mvulana mdogo. Hawakujua lolote, hawakuamini alikuwa ni nabii yeyote, bila shaka hawakuamini.

129 Kamwe hawaamini hilo. Hivi Yesu hakusema, "Ninyi ni kuta zilizopakwa chokaa, ninyi—ninyi mnazipaka rangi kuta za manabii, nanyi ndio mliowaweka humo ndani"?

130 Mwangalieni Yeremia, Isaya, yeyote wa hao manabii, hawakuwatambua mpaka yote yalipokwisha. Ndipo wakati Yohana alipokuja, hawakujua kile. . . Yesu alisema Mwenyewe, "Huyo alikuwa ndiye Eliya aliyenenwa habari zake." Nao walikuwa wamefanya, wamemfanyia yale waliyotaka, na hata wanafunzi hawakujua alikuwa ndiye, Yohana alikuwa ndiye yule Eliya.

131 Ndipo wakati Yesu alipokuja, hawakujua Yeye alikuwa ni Yesu, hawakumtambua kuwa ni Kristo, bali wale waliokusudiwa Uzima wa Milele, "Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu," wanaitambua.

132 Hebu tuteremke, Mtakatifu Patrick, ninyi Wakatoliki mnaomwita Mkatoliki, laiti mngetoa historia yake. Hakuwa Mkatoliki, alimpinga askofu wa Rumi. Hiyo ni kweli kabisa. Shule yake ilikuwa huko Ayalandi ya Kaskazini. Hakuamini katika uongozi huo wa mtu mmoja, aliamini katika uongozi wa Roho Mtakatifu. Naam, bwana. Pia aliamini katika ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kunena kwa lugha, na—na nguvu za Roho.

133 Mtakatifu—Mtakatifu. . . Nilikuwa nikijaribu kusema nini? Columba alifanya jambo lile lile, Mtakatifu Martin alifanya jambo lile lile, Ireneo, jambo lile lile, wote waliamini katika nguvu za Mungu, katika uponyaji wa Kiungu, nguvu za Roho Mtakatifu, hao watakatifu wote wa mwanzoni.

134 Halafu walikuwa na kundi la maaskofu waliokuwa wagumu, nao walitaka kuunda dhehebu, nao wakaliundia kanisa dhehebu na kuchanganya dhambi na ushirikina fulani wa kanisa pamoja, na kuunda dhehebu lao. Kutokana na hayo likaja lile dhehebu mama, kutoka hilo kukaja kila moja ya hayo mengine moja kwa moja kutoka kwake.

135 Someni Ufunuo 17 mwone kama sivyo, yule mama kahaba, na binti zake walikuwa ni malaya. *Malaya* ni nini ila *kahaba*? Kitu lile kile. Ni kitu gani kinachofanya hiyo? Wakifanya uasherati wa kiroho dhidi ya Baba wa kweli, Mume wa kweli, wakichukua mafundisho ya kujibunia na kanuni za imani, wakiwachukua watu, wakiwa wa kawaida, wakiwaingiza katika ibada ya kale, ya kawaida. Tunamwabudu Mungu katika Roho na katika Kweli, Mungu anawatafuta hao kumwabudu. Naam. Hakika, ndivyo ilivyo.

136 Sasa, tunaona ya kwamba Ibrahimu, Ibrahimu alikaa huko nje, alichaguliwa, Kanisa lililoitwa litoke. Basi kumbukeni, Mtu aliyekuwa katika mwili wa mwanadamu, Mtu huyo alikula nyama ya ndama, alikunywa maziwa kutoka kwa ng'ombe, alikunywa mkate na akala sia-. . .akala mkate na kuupaka siagi, akinywa maziwa kutoka kwa ng'ombe, naye Ibrahimu akamwita *Mungu*. Angalieni, chukueni . . . Waangalieni wafasiri, lifuatilieni, angalieni kama hiyo ni kweli, Elohimu, Mungu. Sasa, ninawatakeni mwone, ilikuwa ikiwakilisha kitu fulani, kitu ambacho tunataka kuwaruhusu, hakika, mkione.

137 Sasa angalieni, ndipo tunaona ya kwamba wakati hao watu wawili waliposhuka, hao wahubiri waliposhuka kwenda kuhubiri, Malaika wawili walishuka kwenda kuhubiri Sodoma, kamwe hawakufanya hili, jambo hili, ile ishara, kwamba walishuka wakaenda kule na kuonyesha ishara yao, kwamba walikuja kuwatoa, bali haikuwa ni ishara ile ile Kanisa teule liliyopata.

138 Kanisa teule lilipata ishara nyingine. Na sasa angalia, kile Kanisa huko nje lilichopata, Yule aliyebaki nyuma pamoja na Kanisa teule, mnakumbuka alipokuwa akizungumza? Alisema, "Ibrahimu," akamwita kwa jina lake jipya ambalo Mungu alikuwa amempa, "Ibrahimu, yu wapi Sara?" S-a-r—r-a, jina lake jipya. Mbona, Yeye Ndiye aliyewapa! Naam.

139 Mtu fulani alisema, nimetoa tamshi hilo mara nyingi, kasema, "Ndugu Branham, huamini mtu huyo alikuwa ni Mungu?"

140 Nikasema, "Biblia ilisema alikuwa ni Mungu." Mnaona? Alifanya hivyo. Yeye ni Muumba, anaweza kufanya lolote atakalo. Aliokota tu petroli kidogo, na nurulimwengu, na kalisi, na potashi, na, "*Fiu*!" akapulizia ndani yake, kisha akaingia katika huo mwili, akashuka. Hivyo ndivyo alivyofanya hasa,

aliwafanyia Malaika pale vivyo hivyo. Anaweza kufanya jambo lile lile.

141 Tulitoka wapi? Ni nani aliyeiumba dunia? Alipata wapi nyenzo za kuiumba dunia? Niambieni mahali alipotoka na kuzipata. Dunia yenyewe tunayokalia ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Mimbara hii ni Neno la Mungu, *hii* ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Mungu alilinena, Naye ni Muumba, Naye aliifanya kutokana na vitu ambavyo, sio, havikuwapo hapa kuumba kwavyo, Yeye aliiumba. Ana kusudi, Yeye anaweza kuumba, anaweza kufanya lolote atakalo, Yeye ni Mungu.

142 Ibrahimu alimwita *Mungu*, huyo Ndiye alikuwa. Ibrahimu anapaswa kujua, alizungumza Naye, alikuwa akizungumza Naye maishani mwake mwote, nadhani anapaswa kujua Yeye alikuwa ni Nani. Naam. Hakika. Alimwambia, "*Mimi*, *Mimi* nitatimiza ahadi hii niliyokuahidi." Ni nani Yule aliyezungumza naye huko nyuma? "*Mimi*, *Mimi* Ndimi," Yeye alisema. Basi angalieni, basi wakati . . . Yeye alisema, "Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?" Ibrahimu, si *Abramu*, *Ibrahimu*.

143 Naye Mungu, katika mlango uliotangulia, alikuwa ndiyo kwanza ampe jina hilo la Ibrahimu. Hawakuwa na magazeti wala televisheni na—na kadhalika siku hizo, Ibrahimu alikuwa huko nje peke yake, huko nje, yeye na mke wake na watu wa—wake, watumishi wake. Na kwa hiyo, Mungu alikuwa amemtokea, na kubadilisha jina lake, naye Malaika akamwita *Ibrahimu*, akabadilisha jina la Sarai likawa *Sara*, na kumwita jina lake *Sara*, "Yu wapi Sara, mkeo,?"

144 Alijuaje kwamba hata alikuwa ameoa? Yeye alijuaje, akiwa ni Mgeni, ya kwamba jina lake lilikuwa Ibrahimu? Alijuaje Yeye alibadilisha jina lake kutoka *Abramu* likawa *Ibrahimu*? Alijuaje ya kwamba alikuwa amebadilisha *Sara* likawa *Sara*? Na vipi . . . ? Ama, *Sarai* likawa *Sara*. Alijuaje mambo haya?

Ndipo Ibrahimu akasema, "Yuko hemani nyuma Yako, *huko* nyuma."

145 Akasema, "Nitakuzuru, Ibrahimu." Kwa maneno mengine, "Nilikuahidi ya kwamba nitakupa mtoto huyu, nawe umeliamini Neno Langu, sasa katika muhula wake nitakuzuru, nawe utampata mtoto huyu mchanga."

146 Naye Sara, akisikiliza kwa siri huko nyuma, alisema moyoni mwake, sasa, alisema moyoni mwake, sasa kumbukeni, chini moyoni mwake, "Je, ningekuwa na furaha, mimi mwanamke mkongwe, mwenye umri wa miaka tisini, nyanya, nyanya wa nyanya wa nyanya, na mume wangu, mzee, bwana wangu huko nje, yeye ni mzee, umri wa miaka mia moja, nami hapa umri wa miaka tisini, ati nitakuwa kama msichana tena?" Akawaza, "*Ha*! Hiyo ni ya kuchekesha!" Ndipo akacheka.

147 Basi yule Malaika akasema, "Kwa nini Sara akacheka?" Isitoshe, bali Yeye alisema, akayarudia hayo maneno kwa

Ibrahimu, yale Sara aliyowazia moyoni mwake, "Akasema, 'Inawezekanaje?'" Amina! Haya basi. Ameketi huku mgongo Wake umeelekezwa kwenye hema! Ndipo Sara kweli akaogopa, akaona yale aliyokuwa amefanya. "Kwa nini Sara akacheka, akisema moyoni mwake, 'Nitawezaje kupata raha na mume wangu tena?'" Lakini Maneno Yake yalithibitishwa, Yeye alikuwa ni Mungu.

148 Sasa, ilikuwa ni nini? Sasa, Yesu alirejea kwenye jambo lilo hilo, Naye akasema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu."

149 Sasa angalieni, "Kwa nini usitoke nje na kugongagonga vituo hivyo vikubwavikubwa?"

150 Sikutumwa kwenye vituo hivyo vikubwa; kwa Kanisa teule, huko ndiko. Hao kamwe hawataliamini, ninajua nikisimama hapa usiku nilipokuwa na upambanuzi huo hivi majuzi usiku, na ninauhisi sasa hivi, kuna wengi hapa ndani wasioamini hilo. Usiniambie, ninaweza kulitaja jina lako. Hiyo ni kweli. Usiniambie. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, ninajua ugonjwa wako, Mungu anaweza kuniambia papa hapa ugonjwa wako, bila shaka. Ninauhisi. Kwa nini unajaribu kujifanya mnafiki juu yake? Kwa nini usiwe kile ulicho hasa? Jambo moja, unaogopa, sikulaumu, neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe.

151 Lakini ninawatakeni mjue ya kwamba Maandiko si itikadi za kimafumbo, kama baadhi yenu wahubiri mnavyodhani ndivyo yalivyo, Si telepathia. Mungu airehemu nafsi yako yenye dhambi! Huhitaji mimbara, unahitaji madhabahu. Hiyo ni kweli. Jipatanisheni na Mungu. Kumbukeni, neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe katika ulimwengu huu, wala ulimwengu ujao. Sasa, unasema, "Si mimi." Usiniambie wewe ni nani, najua. Unaona? Naam, bwana. Kwa hiyo sasa, sikilizeni, ninawaonya tu. Kumbukeni, Mungu aliahidi hilo lingetukia. Amina.

152 Angalieni, Yeye alisema... Angalieni, ilikuwa ni nini? Mungu katika mwili wa mwanadamu. Naye Mungu angejiwakilisha Mwenyewe, tena, katika mwili wa kibinadamu, kabla tu ya kuja kwa Mwana wa Adamu. Mwili gani? Mwili wako, mwili wangu. Mungu, akishuka kutoka Mbinguni, Mungu akitamani ushirika. Jinsi watu...! Inaonekana kana kwamba kuna theolojia nyingi sana ya kiakili juu yake, unakosa kupata upambanuzi wa Roho.

153 Kama vile jamaa fulani alivyokuwa akijaribu kuniambia hivi majuzi kuhusu kuweko na Miungu watatu, Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. *Baba* ni kipindi cha wakati wa Baba, haikuwa ni Miungu watatu, ni ofisi tatu za Mungu yeye yule, Ubaba, Uwana, Roho Mtakatifu, Mungu yeye yule katika kila Mmoja. Haikuwalazimu kuwa na Baraza la Nikea kwa ajili ya jambo hilo. Ni Mungu, Mungu yeye yule daima, Mungu mmoja.

Alikuwa katika Ubaba, hiyo ndiyo sababu Mathayo alisema, "Mkawabatize kwa jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Si Miungu watatu, Mungu mmoja katika ofisi tatu, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sifa tatu. Bila shaka.

154 Alikuwa katika Nguzo ya Moto kama Mungu, Yehova, Yeye, hakuna mtu angaliweza kumgusa, dhambi ilikuwa mbali sana Naye, asingeweza kuwakaribia. Ndipo akaja na kumtia uvuli bikira, akaumba Seli ya Damu katika tumbo lake la uzazi, Mtoto akatokea, Yesu, mwili mtakatifu, si Mmataifa, wala Myahudi, Damu ya Mungu Mwenyewe.

155 Ndipo Roho Mtakatifu mkuu akashuka kutoka Mbinguni, Roho wa Mungu, kama hua akishuka, akaenda juu Yake, "Huyu ni Mwanangu mpendwa," kwa tafsiri sahihi, "ninayependezwa kukaa ndani Yake." "Baba Yangu anakaa ndani Yangu." Mwulize mfasiri yeyote mzuri wa Maandiko uone kama hilo haliko katika Kiebrania. Naam, bwana. "Ninayependezwa kukaa ndani Yake."

156 Yesu alisema, "Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe. Si Mimi nizitendaye hizo kazi, bali Baba Yangu, Yeye anakaa ndani Yangu, Imanueli." Si Mungu mwingine *huko* juu, na Mwingine *hapa*, na Mwingine *hapa* chini, huo ni ukafiri, Mungu mmoja katika ofisi tatu. Mungu Baba Mwenyezi alishuka na kukaa ndani ya Mwanawe Kristo Yesu; aliyatoa maisha Yake akijaribu kujikuta Mwenyewe amerudi kwenye ushirika na watu Wake, akijaribu kurudi.

157 Hakuna mtu angaliweza kuilipa hiyo gharama, wenye dhambi wote. Naye Mwanawe Mwenyewe alifanywa dhambi kwa ajili yetu kuziondoa dhambi zetu, na hilo lingemfanya Baba Mungu yeye yule katika umbo la Roho Mtakatifu ashuke na kukaa ndani yetu, na kufanya kazi kupitia kwetu, kama alivyomfanyia Mwanawe aliyeumbwa. Amina. Huo hapo ukweli wako.

158 Mna upande mmoja wa barabara, *hapa*, ukisema, "Mungu ni *mmoja*, kama vile kidole chako kilivyo *kimoja*, hawezi kuwa Baba Yake Mwenyewe."

Tunao *hapa* wakisema, "Yeye ni Miungu watatu mbalimbali."

159 Vema, kama Yeye ni Miungu watatu mbalimbali, basi Mungu Roho Mtakatifu, na Mungu Baba ni Watu wawili tofauti, basi bikira alitiwa mimba na Roho Mtakatifu. Ni yupi aliyekuwa Baba Yake? Ana Baba mmoja. Roho Mtakatifu na Mungu ni Roho yeye yule, hiyo ni kweli. Ndipo katika hilo . . .

160 Loo, si fumbo. Kama alikuwa na . . . Kama—kama mtu alikuwa . . . Kama Wawili walikuwa Baba Yake, basi Yeye ni mwana haramu, hakika kabisa, kiroho. Mnaona, yote yamevurugika, hayana maana. Jambo pekee, ni kwamba watu hujaribu kuliwazia kwa kichwa chao, badala ya kuuacha moyo

wao umwendee Mungu. Naye Mungu angewafunulia mambo hayo, kama tu ukimruhusu afanye hivyo. Naam, bwana.

161 Hawezi kuwa Baba Yake Mwenyewe, Yesu asingeweza kuwa Yesu mmoja, Mungu mmoja, wote namna hiyo, Yeye aliumbwa na Mungu Baba. Kweli. Naye Mungu Baba alikaa ndani Yake kusudi atumie Damu Yake kwa ajili ya utakaso, na kulisafisha Kanisa Lake kwa Roho yuyo huyo, apate kuishi katika Kanisa Lake, kufanya kazi na ishara, na kutimiza Maandiko aliyoahidi, "Katika siku za mwisho, kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . .? . . .

162 Jambo ndilo hilo, kujifunza kile mtu mwingine . . . Yesu alimwambia nini Petro? "Heri wewe, Simoni, mwana wa Yona, hukujifunza hili katika seminari, mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia hili. Na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda." Hiyo ndiyo sababu Yeye alimpa funguo, alikuwa na ufunuo, ni kweli iliyofunuliwa.

163 Loo, ninii, hayo—hayo mambo madogo wanayopigania na kutengana, inaonyesha si ya Mungu, la sivyo wasingetengana namna hiyo. Kwa nini msije pamoja na kuwa ndugu, dada? Acha nguvu za Mungu zitende kazi miongoni mwenu, zitafanikisha yote. Mungu ndiye Mwalimu wa Kanisa, Roho Mtakatifu, hiyo ni kweli. Haikubidi kutumia maisha yako yote ukijaribu tu kujifunza kitu kama hicho, jambo bora kuliko yote ni kujua umeokoka na kuita- . . . uanze kutembea na Mungu, yale anayotaka ujue, Yeye atakufunulia.

164 Huyo hapo Mungu Mwenyezi, aliyefanyika mwili katika ukumbusho ambao . . . Yesu alisema, "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, *ndani yenu*, hata ukamilifu wa dahari," kote kote hata mwisho wa ulimwengu. Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.

165 Yupo hapa. Ni Kristo akifanya kazi ndani yako, na mimi, na wengine wetu, akijaribu kulileta Neno Lake pamoja kuthibitisha, na kulitimiza Neno Lake. Kwa nini Yesu akawaponya wagonjwa, Mathayo 12? Mathayo 8, ninaamini ndiyo. Yeye alisema, "Lipate kutimia lile lililonenwa na nabii." Neno la Mungu linahitaji kutimizwa, hii ndiyo saa.

166 Telepathia, wanaiita, waliita kitu kile kile pale, ibilisi. Akasema, "Haisameheki kumwita Roho wa Mungu anayetenda kazi, kitu kama hicho." Ninawatakeni mfikirie hilo kabla hamjaanza kufanya maamuzi yenu. Hiyo hapo huduma mpya ambayo Mungu ameithibitisha, nasi tunajua kwamba ni kweli ya Mungu, lakini *kwa namna fulani* haitafanya kazi hapa—hapa

Marekani, inafanya kazi mahali pengine, sasa, kubwa kuliko tulizo nazo hapa.

167 Lakini mnaona, tulininii tu—tulitenda dhambi tu tukamaliza siku yetu ya neema, hakuna lingine. Nilibashiri hilo katika mwaka wa 1956, na imekuwa hivyo tangu wakati huo, ikianguka daima. Mnaona? Lakini Mungu ataliondoa Kanisa hilo teule, Yeye—Yeye anawajibika kufanya hivyo, alisema angefanya hivyo.

168 Sasa, mwangalieni yule Malaika aliyegeuza mgongo Wake, akamwambia Sara yale aliyokuwa akiwazia. Kama hilo si Neno la Mungu, silijui. Biblia ilisema katika Waebrania 4 ya kwamba "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, na hata ni Mtambuzi wa mawazo ya moyo, nia." Kweli, Hilo huyatambua, ni Neno la Mungu. Nalo Neno la Mungu liko ndani yako kama utaliruhusu Neno, kwa sababu Yeye ni Neno.

169 "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu." Mnaona hilo? Ndipo Neno lilo hilo, Kristo, ile ahadi, Roho Mtakatifu, mnamwita Nafsi ya tatu katika utatu, hilo ni sawa, hivyo ndivyo alivyo, Kristo, Roho Mtakatifu ndani yenu, Yeye alikuwa katika Nguzo ya Moto wakati mmoja, kisha akaja, akafanyika mwili, sasa Yeye amekuja katika mwili wako.

170 Yeye anafanya nini? Mungu akijidhili, akijaribu kuwakaribia watu Wake kusudi aweze kupendwa na kuabudiwa. Nasi, katika Wakati wa Laodikia, tumemtupa nje, Yeye anabisha, akijaribu kurudi ndani.

171 "Wote niwapendao, nawakemea na kuwarudi, tubuni," Yeye alisema. Sisi hapa. Huyo ni Mungu, huyo ni Mungu Baba yetu katika umbo la Roho Mtakatifu akijaribu kurudi maishani mwetu kututawala. Hana budi kuwa na Kanisa la kufanya, kama nilivyosema jana usiku, lile Jiwe la Kufunika lije juu, halina budi kuja pale kikamilifu, nalo Kanisa halina budi kuvuta liingie katika ukamilifu.

Unasema, "Ukamilifu?"

Hivyo ndivyo alivyosema, "Iweni wakamilifu, kama Baba Yangu aliye Mbinguni alivyo mkamilifu," Mungu.

172 Hebu na tuchukue wazo fulani, hebu tuchukue ninii—hebu tuchukue mfano mdogo hapa kwa dakika moja. Angalieni hili, sasa, kama nilivyokuwa nikisema asubuhi ya leo, kama mzabibu una uhai wa mzabibu ndani yake, utazaa zabibu.

173 Sasa, Nguzo hii ya Moto iliyoambatana na watoto nyikani, mtu yeyote anajua ya kwamba Huyo alikuwa ni Mungu. Tunajua ya kwamba Huyo alikuwa ni Mungu, Yeye alimwambia Ibrahimu, uh, alimwambia Musa, "MIMI NIKO AMBAYE NIKO. Nami nimeyaona mateso ya watu Wangu, na kusikia

kuugua kwao kwa sababu ya wasimamizi, nami nimeshuka kuja kuwakomboa."

174 Sasa, hiyo ilikuwa ni Nguzo ya Moto kwenye kile kichaka. Mnaamini hilo? Malaika wa Agano. Vema, ilikuwa ni . . . Ilishuka juu ya Mlima Sinai na kuandika zile amri. Hata kama mnyama aligusa, ilibidi auawe. Ilikuwa ni kitu gani? Kwa sababu hapakuwapo na dhabihu ya dhambi, mnyama.

175 Mnaona, wakati Agano la Kale, walipotoa sadaka ya dhambi, walimchukua mwana-kondoo mdogo, wakaweka mikono yao juu yake, wakaungama dhambi zao, kisha wakakata koo lake. Basi wakati maskini jamaa huyo alipokuwa akifa, akirusha mateke, na kulia, mbona, damu ilijaa kila mahali mikononi mwa mwabuduo, na ndipo akahisi mauti yakimtoka mnyama huyo wakati akijinyosha na kufa, naye alijua ya kwamba mnyama huyo alikuwa akifa mahali pake.

176 Lakini Biblia ilisema alitoka akiwa na tamaa ile ile aliyokuwa nayo wakati alipoingia, maana mnaona, wakati chembe hiyo ya damu ilipovunjwa, roho hiyo ya mnyama isingeweza kurudi na kuambatana na roho ya mwanadamu. Mnyama hana nafsi, kwa hiyo wasingeweza kurudi, kwa hiyo basi alitoka nje akiwa na dhamiri ile ile. Lakini wakati mtu, kwa imani, anapokuja, anaweka mikono yake juu ya kichwa cha Yesu Kristo na kuhisi mateso Yake kwa ajili ya dhambi zako, basi wakati Chembe hiyo ya Damu ilipovunjwa pale Kalvari, si kwamba tu uhai wa mwanadamu ulirudi, bali Uhai wa Mungu unarudi kutoka kwake na kukufanya mwana na binti wa Mungu.

177 Angalia wakati Nguzo hiyo ya Moto ilipofanyika mwili, na kukaa miongoni mwetu. Tulimpataje hivi majuzi usiku, yale aliyofanya? Jinsi walivyomjua Yeye, kwa kuyatambua mawazo ya moyo. Walijua Huyo alikuwa ni yule Nabii ambaye Musa alinena habari zake, Yeye alidai kuwa huyo, walijua alikuwa hivyo, hivyo ndivyo alivyokuwa. Sasa, Yeye aligeuka akawa Huyo tena, mlijua hilo?

"Loo, la, Ndugu Branham."

Loo, naam, Yeye alifanya hivyo, pia. Yeye alisema, wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye alisema, "Nimetoka kwa Mungu, na ninaenda kwa Mungu." Hiyo ni kweli?

178 Na baada ya kufa, kuzikwa, kufufuka, na kupaa Juu, Sauli wa Tarso alikuwa akienda zake Dameski siku moja kuwafunga gerezani watu waliokuwa wakiabudu, na kwa ghafla Nuru kuu ikamulika mbele yake, naye akaanguka chini. Basi hiyo Nuru kuu ilikuwa angavu sana hata ikayapofusha macho ya Sauli, alikuwa kipofu kwa muda. Naye akasema, "Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?"

Akasema, "U nani Wewe, Bwana?"

Akasema, "Mimi ni Yesu." Alirudi kwenye Nguzo ya Moto tena.

179 Nasi tuna picha Yake moja kwa moja pamoja nasi, kanisa la Kipentekoste. Haleluya! Sasa, ni Roho yeye yule? Je, ni Nguzo ile ile ya Moto? George J. Lacy, mkuu wa FBI, alama za vidole na hati, unaninii . . . hiyo hapo hati yake iliyoandikwa juu yake, kasema, "Nuru iliigusa lenzi." Kasema, "Hakuna saikolojia kulihusu, maana jicho hili la kimitambo la kamera halitapiga picha saikolojia." Iligusa lenzi.

180 Ilipigwa nyingine papa hapa mahali pengine, zilipigiwa Uswisi na Ujerumani. Wanataka kujua kama *sinema* zao zingeipiga, zile kamera kubwa za Kijerumani zikatolewa, nami nilikuwa nimesimama pale, nikasema, "Bila shaka, kama Mungu atalijalia."

Mimi huyu nikija pale na nilikuwa nikizungumza, nami nikasema, "Sasa, Hiyo inakuja."

181 Naye huyu Mjerumani, akisimama tu pale, angezungusha picha zake, akizipiga, basi alipofanya hivyo, ilionyesha Roho Mtakatifu akishuka, ikaonyesha wakati Yeye . . . Ikamwonyesha mtu huyo pale huku ukosi wake umepinduliwa, nami nikamwambia, kwa Roho, "Umesimama hapo kama kasisi, bali wewe si kasisi. Wewe hata si Mjerumani," Nikasema, "wewe ni Mwitaliano, wewe ni kiongozi wa wakomunisti elfu ishirini. Ulikimbia na chama, una kituo kidogo cha watoto yatima huko juu milimani. Hukula kiamshakinywa chako kwa sababu una ugonjwa wa tumbo. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI." Nikasema, "Kula kiamshakinywa chako, Yesu Kristo anakuponya."

Akaketi chini na kuanza kula kwa pupa alivyoweza, akilia.

182 Ndipo wakapiga picha ya Roho Mtakatifu akishuka, wakati aliposhuka, wakati alipokuwa akitia mafuta, na wakati alipoondoka, moja kwa moja mchana, ikisimama pale. Ni kitu gani? Sio saikolojia! Hivi uko mbali sana na Mungu hivyo, ndugu yangu? Si saikolojia, hiyo kamera inajua zaidi kulihusu kuliko wewe.

183 Sasa, ni Roho Mtakatifu? Vema, kama anatenda kazi za Yesu Kristo, ni Roho yeye yule aliyekuwa juu Yake. Basi mnaweza kuwa na hakika ya kwamba ninyi mnaomwamini Mungu, na mnaamini mna Roho Mtakatifu, kwamba Huyo ni Roho Mtakatifu yeye yule, kwa sababu anafanya jambo lile lile alilofanya wakati alipokuwa juu ya Mwana halisi wa Mungu. Anapokuja juu ya wana na binti wa kufanywa wana wenye mamlaka, anafanya jambo lile lile alilofanya kule.

184 Kama ningekwambia nilikuwa na roho ya John Dillinger, ungenitarajia niwe na bunduki mbili kubwa, kama ningekuwa na roho yake. Kama ningekuwa na roho ya msanii, ungenitarajia kuchora picha za mawimbi huko nje, niyashike hayo mawimbi

mazuri na kuyapaka rangi; kama ningekuwa na roho ya msanii, ningeweza kufanya hivyo. Kama ningekuwa na roho ya makanika, ningeweza kusikiliza gari lako na kukwambia shida yake.

185 Kama nikiwaambia nina Roho wa Kristo, basi nifanye kazi za Kristo. Hamwezi kuniamini mimi, mbona, aminini zile kazi, aminini ya kwamba Mungu alimtuma. Kwa sababu sijiungi na madhehebu na kadhalika, msipotaka kuamini kwa sababu hiyo, basi aminini kazi zenyewe na mwokoke. Hiyo ni kweli.

186 Ninajua ni vigumu, sijui ni kwa nini ninalisema, lakini ha—haina budi kusemwa mahali fulani. Haina budi kuwa ni kweli, haina budi kufanywa ijulikane. Kwenye Siku ya Hukumu, nitakutana nanyi kule, katika Jina la Bwana Yesu, Yeye angali atathibitisha ya kwamba ni kweli, bali liko katika Biblia Yake, "Na mbingu na nchi zitapita, Neno Langu halitapita kamwe." Amina. Mrudieni Mungu, huo ndio wito. Mrudieni Mungu tena.

187 Ibrahimu alimwita *Elohimu*. Akaugeuza mgongo Wake, kuwaonyesha kile Mungu alichofanya wakati huo, maana Ibrahimu alitambua ya kwamba Huyo alikuwa ni Mungu katika mwili wa kibinadamu akiishi papa hapa pamoja naye, akizungumza naye.

188 Yesu alisema, kwa maneno mengine, Yeye alisema kuninii . . . Mnajua kile Malaika wa Bwana alichofanya huko chini Sodoma? Angalieni kile Wasodoma walichokuwa wakifanya, walikuwa wakinunua, na kujenga, loo, jamani, makondrakta kote nchini, majengo.

189 Uliwahi kuona wakati kama huo? Hata siwezi kwenda kuwinda sungura tena nyumbani, ninii, yote ni miradi ya ujenzi wa nyumba ambapo shamba lilikuwa. Sijui tutafanya nini tupate kula. Kujenga, kujenga, hivyo ndivyo hasa Yesu alivyosema ingetukia. Je, Yeye alisema jambo hilo? Walikuwa wakioa, wakiolewa, kama katika siku za Nuhu. Angalieni Reno, Nevada, na mwangalie hapa.

190 Taifa hili lingekuwa bora zaidi kama lingekuwa—kama lingekuwa, afadhali nisiseme hilo. Vema. Lakini, hata hivyo, ingekuwa afadhali kuwa na wake watatu au wanne kuliko, afadhali nisimame mbele za Mungu pamoja na wanawake watatu niliowaoa, ama wanawake watano niliowaoa wakisimama karibu nami, kuliko kusimama pale na mke mmoja, na kuzurura na mke wa mwanamume mwingine. Naam, bwana. Ningekuwa na nafasi nzuri zaidi mbele za Mungu.

191 Huwezi kuwalazimisha wenye dhambi kuchukua wajibu wa Mkristo na kufanya hivyo, hawawezi kufanya hivyo mpaka wazaliwe mara ya pili. Hiyo ni kweli. Tuko mbali sana na kuwa taifa la Kikristo. Tungefunguaje kila klabu ya pombe haramu iliyo kwenye kona, na kuendesha mambo jinsi tufanyavyo,

kujiita wenyewe Wakristo? Hao si Wakristo, si zaidi ya vile nguruwe anavyojua kuhusu matandiko ya mwanamke.

192 Vema, usingeweza kuuita huo Ukristo, sisi si taifa la Kikristo, la, bwana. Kunao Wakristo *katika* taifa hili, bali si taifa la Kikristo. Ninamshukuru Mungu kwa ajili ya Wakristo walio humu ndani. "Si wote waniambiao, 'Bwana, Bwana,' watakaofanya. . . watakaoingia, bali yule afanyaye mapenzi ya Baba Yangu aliye Mbinguni," huyo ndiye anayeingia.

193 Kuna faida gani kuwa nusu? Kuna faida gani ya kuwa na kanisa vuguvugu? Ama uwe moto kabisa, au—au baridi kama barafu. Usidai Pentekoste, isipokuwa unaishi Pentekoste, usiruke juu zaidi ya unavyoishi. Hiyo ni kweli. Ni aibu, inaleta fedheha juu ya hao wengine. Zaidi sana, si vilabu vya pombe haramu vinavyomdhuru asiyeamini, ni watu hawa wanaodai kuwa na *kitu fulani* na kutenda kama walimwengu, hilo ndilo jiwe la kujikwaa.

194 Kanisa linalopaswa kuwa linawaka moto kwa ajili ya Mungu, na kwenda huku na huku wakimwita Roho yeye yule wa Mungu ajaye, wakisema, "Ni—ni fumbo, ni telepathia, ni yote *haya*, *yale*, ama *mengineyo*," kwa sababu sisi si wa dhehebu lao. Jioneni aibu! Mungu azirehemu nafsi zenu zenye dhambi. Mtakutana na hiyo kwenye Siku ya Hukumu, na labda, kabla ya kuingia Hukumuni, hiyo ni kweli, maana Mungu aliahidi hilo.

195 Loo, tuko katika wakati mbaya sana, marafiki. Loo, ulimwengu unazama, taifa linakufa.

> Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
> Ishara ambazo manabii walitabiri;
> Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa na hofu;
> "Rudini, makwenu, Enyi mliotawanyika."
>
> Siku ya Ukombozi imekaribia,
> Mioyo ya watu inazimia kwa hofu;
> Jazweni na Roho wa Mungu, taa zenu zimetengenezwa na ni safi,
> Angalieni juu! Ukombozi wenu unakaribia.

196 Loo, ni siku ya jinsi gani tunayoishi! Vipi kama Paulo angekuwa anaishi katika siku hii? Vipi kama Mtakatifu Petro angekuwa anaishi katika siku hii, na kuona Pentekoste katika hali hiyo? Angewatikisa, bila shaka angewatikisa, maana alikuwa na Roho Mtakatifu ndani yake, bila shaka angewatikisa.

197 Sasa angalieni, ninataka kuwaonyesha yale Mungu aliyowaahidi hao washindi, yale Mungu aliyowafanyia hao washindi. Nina dakika kumi na tano tu kuwaachilia kwa wakati. Hebu tuone kile Mungu alichofanya, papo hapo, wakati Ibrahimu alipotambua hilo, na kusema, "Naam, huyo ni Mungu," akamwita *Elohimu*, "Bwana Wangu," si "Bwana

Zangu," "Bwana Wangu." "Bwana wangu," akasema, herufi kubwa za B-w-a-n-a. Angalieni kile alichomwita Yeye.

198 Na wakati alipomtambua, na kujua ilikuwa ni kitu gani, naye akaomba rehema kwa ajili ya *idadi fulani* ya watu, *idadi fulani* ya watu, kisha hatimaye akatoka hamsini hadi kumi, bado asingeweza kuwapata katika—katika Sodoma, la sivyo Yeye angaliuokoa huo mji, lakini Yeye hata asingeweza kuwapata katika kanisa lote, huko chini kusingekuwako na watu watano, ama, kumi waaminifu, alitoka tu na watatu, alikuwa na wanne, na mmoja wao akageuka, akaangalia nyuma, mke wake. Hakutaka kuacha vitu vyake vizuri vya Hollywood, na mahali pake pazuri, mwajua. Naye akageuka akawa nguzo ya chumvi.

199 Usiangalie nyuma. "Yeye awekaye mkono wake kulima kwa plau, na hata akageuka kuangalia nyuma, hafai kwa kulima kwa plau." Hayo ndiyo yaliyo katika kanisa hili, ndugu. Ukiweka mikono yako kulima na kujiita Mpentekoste, aliyejazwa na Roho Mtakatifu, acha kuuangalia ulimwengu, na kutenda kama walimwengu, na kujipamba kama walimwengu, pamoja na upuuzi kama huu wote, na kuwa na mambo ya kilimwengu, na kukaa nyumbani ukiangalia televisheni, badala ya kuja, mkutano wa maombi, huku wenye dhambi wanakuja madhabahuni, na kamwe hawapati msukumo kutoka kwa mtu yeyote, wanakuja, haiwavutii, tena.

200 Hebu niwape onyo dogo, Ezekieli mlango wa 9, Biblia ilisema, ilimwambia mwenye kutia alama kwa—kwa Roho Mtakatifu, "Piteni katikati ya mji, mkawatie alama wale wanaougua na kulia kwa ajili ya machukizo yanayofanywa mjini." Ni wangapi waliowahi kuisoma? Hakika. "Usimtie alama mtu mwingine ila hao." Hesabuni kwenye vidole vyenu na mniinulie, ni watu wangapi, mtu yeyote aliye katika jengo hili anaoweza kuwatia alama wanaougua na kulia mchana na usiku kwa ajili ya machukizo yanayofanywa katika mji huu? Sioni kidole.

201 "Watie muhuri wale *tu* wanaougua na kulia kwa ajili ya machukizo yanayofanywa mjini." Wengi wao hata wanaogopa kuhubiri dhidi yake, wengi wao wanaogopa. Mungu atupe watu wenye uti wa mgongo badala ya mfupa wa shingo ya kuku. Naam, bwana. Tupe Yohana Mbatizaji mwingine, mtume aende, mpake mafuta kwa Roho Mtakatifu, ambaye hatacheza, bali atadumu na Neno. Na kama akidumu na Neno, asiogope, Mungu ataliunga mkono Neno Lake.

202 Nimepitia katika mahali pagumu pa kila namna, ambapo pepo, na kadhalika waliinuka, niliwaona wakipofushwa, wakibwagwa chini, na kadhalika. Msiogope, kaeni papo hapo kwenye Neno, angalieni yale Mungu afanyayo; hakikisheni tu kwamba mmejipatanisha na Mungu. Dumuni na hilo Neno, kisha mwangalie kinachotukia.

203 Kama Ndugu Arganbright ameketi karibu, angeweza kuwasimulia hiyo hadithi, nilikuwa nikiwazia sasa juu ya wale wachawi kumi na watano upande mmoja, na kumi na watano upande mwingine, walioitisha dhoruba kulipua hema huko Uswisi, ama, ninaamini ilikuwa ni Ufara-. . . Ujerumani. Walitaka kulilipua hema, walitwambia walikuwa wanaenda kulilipua, na kuketi hapo na kukata hayo manyoya na kuanza kufanya vitimbi, "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, *blrr*, *blrr*, *blrr*. Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," maneno matatu makuu, walisema. Yote namna hiyo, na hii hapa dhoruba inakuja.

204 Ndugu Arganbright atawaambia vivyo hivyo, ambapo makumi ya maelfu ya watu, hilo hema likiruka juu chini. Nikasema, "Omba, Ndugu Arganbright." Nikasema, "Ndugu Lowster, usifasiri hili."

205 Nikasema, "Baba wa Mbinguni, nilishuka kutoka kwenye hiyo ndege hapa juu katika Jina la Yesu Kristo, kwa sababu Wewe ulinituma hapa, uliahidi ya kwamba utanishughulikia. Nifanye nini katika kisa kama hiki? Ninakemea dhoruba hii, katika Jina la Yesu Kristo."

206 Katika sekunde moja kamili tufani hiyo ikagawanyika moja kwa moja juu ya hema, na kurudi nyuma, ngurumo zikaanza kurudi nyuma, namna *hiyo*, ndipo maelfu wakakimbilia madhabahuni wapate kuokoka, nao wachawi wakashindwa.

207 Mtu huyo aliyeketi mkutanoni, akijaribu kunirushia moja ya hizo laana, kunifanya nibweke kama mbwa, apate kujigamba mle ndani, yeye hakujua, akiketi pale. Nami nikaendelea kuhisi roho hiyo ya kipekee, nikawaza, "Nachukia kumtaja huyo kwa sababu yeye ni rafiki ya mtu fulani."

208 Yesu akasema, "Acheni vikue pamoja, mtang'oa ngano mnapoyang'oa magugu." Nami nikaendelea kwenda kule, naye akaendelea.

209 Baada ya kitambo kidogo Roho Mtakatifu akaendelea kusema nami, nikageuka, nikasema, "Ewe mdanganyifu! Kwa nini uje mkutanoni, ibada ya Mungu kujaribu kumdanganya mtu?" Naye akaendelea kuangalia kote, kana kwamba nilikuwa nikizungumza na . . . Nikasema, "Ni wewe ninayekuzungumzia." Nikamwita jina lake. Nikasema, "Kwa sababu ulimfanyia Roho wa Mungu hivi, mtu fulani atakubeba akutoe hapa." Naye angali amepooza. Mnaona?

Akaandika barua, na kusema, "Nifanye nini?"

Nikasema, "Tubu!"

Kasema, "Njoo, uniondolee hili."

210 Nikasema, "Sina chocho-. . . Kamwe sikuwa na uhusiano wowote na hilo janga kukupata, ulijiletea mwenyewe. Biblia ilisema, 'Ni afadhali jiwe la kusagia lifungiwe shingoni mwako, ukatoswe katika kilindi cha bahari, kuliko kuwaudhi wapakwa

mafuta wa Mungu.'" Hiyo ni kweli. Tumepoteza kicho chetu kwa Mungu, heshima kwa Wakristo. Loo, jinsi tunavyopaswa kumrudia Mungu!

211 Angalieni kile Mungu alichomwonyesha Ibrahimu hapa kwa sababu aliamini Neno, angalia kilichotukia. Yeye alimfanyia nini Sara? Mnajua kile alichowafanyia Sara na Ibrahimu? Ikionyesha yale atakayoufanyia Uzao wote wa Sara na Ibrahimu, Uzao wa Ibrahimu, yale atakayofanya. Mnajua yale aliyofanya? Angalieni walichofanya mara baada ya hayo, walifanya safari ndefu kutoka mahali walipokuwa wamepiga kambi, huko juu, Sodoma, kote kote mpaka Gerari, kuingia huko chini katika nchi ya Wafilisti, yapata maili mia tatu.

212 Huo ni mwendo mrefu sana kwa mzee wa miaka mia moja, na maskini bikizee mwenye shali ndogo mabegani mwake, akitembea namna *hii*, kutembea maili mia tatu. Haikuwa hivyo, Yeye aliwageuza wakawa kijana mwanamume na kijana mwanamke. Ninaweza kulithibitisha, Yeye aliwageuza. Basi hiyo ni ahadi kwa Uzao wake wote utakaolichukua Neno Lake, na kulishikilia namna hiyo.

213 Alimgeuza Sara kuwa msichana ili aweze kumzaaa mtoto huyo. Ninataka kusema jambo fulani, sasa, ninyi humsikiliza daktari wenu, mimi ni ndugu yenu. Sasa angalieni, kama alikuwa mzee hivyo, ingembidi Yeye kuuimarisha moyo wake, la sivyo asingeweza kuingia katika utungu wa kuzaa, mwanamke mwenye umri wa miaka tisini, hiyo ni kweli, ingembidi kuutia kiraka moyo wake.

214 Mishipa ya maziwa kutoka kwenye titi lake ilikuwa imekauka. Hawakuwa na . . . Wanawake hawakuvuta sigara siku hizo, kwa hiyo walimlea tu mtoto wao kwa matiti yao, mnaona, wala hawakumpa maziwa ya ng'ombe, kwa hiyo i—i—iliwabidi kuwalisha kwa matiti yao. Nayo mishipa ya maziwa ilikuwa imekauka. Angalieni tu ni hali ya jinsi gani! Ilimbidi kumtia viraka. Mungu hatii kiraka, Yeye hufanya upya. Naam.

215 Ninaweza kumwona Sara akigeuka kuwa mwanamke wa kupendeza, yapata umri wa miaka ishirini na mitano; ninaweza kumwona Ibrahimu yapata umri wa miaka ishirini na mitano, ama thelathini.

Ninaweza kumsikia Sara akisema, akiamka asubuhi moja, akisema, "Mpenzi, hivi ulijua, nundu hiyo inatoweka mabegani mwako?"

216 Ninaweza kumsikia akisema, "Mpenzi, hayo macho mazuri, ya hudhurungi uliyokuwa nayo, yamerudi. Nayo rangi inarudi kwenye nywele zako tena." Loo, jamani! Naam.

Sasa, unasema, "Sasa, Ndugu Branham!"

217 Ngoja kidogo, ngoja kidogo, unaona, Biblia ni Hadithi ya upendo kwa mwaminio. Sasa, ninapoenda ng'ambo, Bibi

Branham ananiandikia barua, naye akasema, "Mpenzi Billy, nimeketi hapa usiku wa leo, sina budi kuwalaza watoto kitandani, ndiyo kwanza nimalize kukuombea, ninajua ya kwamba Mungu anakubariki."

218 Mnaona, hivyo ndivyo anavyosema, bali ninasoma moja kwa moja katikati ya mistari, ninampenda, mnaona, ninajua kile anachozungumzia. Hataniambia yote juu yake, lakini bila shaka ninajua kwa vyovyote vile, jinsi anavyoandika.

219 Vema, hivyo ndivyo unavyoisoma Biblia, katikati ya mistari. Mungu ana ninii . . . Hiyo ndiyo sababu aliificha kutoka kwa macho ya wenye hekima na akili, hao wanaosema, "Nina Ph.D., D.D.D." Unajua D.D. inawakilisha nini? Mbwa aliyekufa. [Kiingereza: Dead dog—Mfa.] Kwa hiyo, nakwambia, ndugu, kile, hatuhitaji hizo siku hizi, tunahitaji, si *theolojia* fulani, bali *elimugoti* ndiyo tunayohitaji. Naam. Vema, Biblia ilimwita *mbwa bubu*, kwa hiyo ingekuwa mbaya tu, mnaona, ilisema walikuwa ni mbwa bubu, ma-D.D.

Sasa, angalieni, alikuwa ndiye huyo hapo ndani.

220 "Nilipata *hii* na nina *ile*." Vema, hilo ni sawa, ninapenda kuwa na Yesu. Walitambua kwamba Petro na Yohana walikuwa wasio na elimu wala maarifa, lakini iliwabidi watambue kwamba walikuwa pamoja na Yesu. Hakuna mmoja wao angaliweza kuandika jina lake, ama chochote kile, bali walijua walikuwa pamoja na Yesu, hivyo ndivyo inavyotupasa kufanya, kujua ya kwamba wamekuwa pamoja na Yesu.

221 Sasa, unaposoma Biblia, Yeye amelificha kutoka kwa macho ya wenye hekima na akili, na atawafunulia watoto wachanga, wale watakaojifunza, kwa hiyo unapoanza kusoma hili hapa, sasa angalia kinachotukia, kuwaonyesha ya kwamba hivyo ndivyo alivyofanya. Jambo la kwanza . . .

Sasa, mnasema, "Loo, Ndugu Branham, walikuwa tu . . ."

222 La, Biblia ilisema walikuwa na umri mkubwa, hiyo ni kweli, walikuwa na umri mkubwa. Sasa, ndugu yangu mshika sheria, sitaki kukufinya sana, bali ninawatakeni mjue ni—ningali ninaweza kufinya kidogo tu kwa Neno, mnaona. Sitaki kuwaudhi, bali nawatakeni mwangalie yaliyotukia.

223 Akashuka kwenda Gerari, na ndipo alipofika huko chini, nitachukua upande wenu wa hilo, huyu hapa maskini nyanya anakuja, karibu umri wa miaka mia moja, kofia ndogo iliyojaa mavumbi, na shali ndogo, mwajua, akipepesuka. Nanyi mwajua, Abimeleki huko chini Gerari, alikuwa ni mfalme, naye alikuwa akitafuta mke, na hao wanawake wote warembo wa Kifilisti, lakini alipomwona maskini nyanya, alisema, "Huyo ndiye nimemngojea!"

224 Loo, Ibrahimu alisema, "Mimi . . . Nipe fadhili zako, useme wewe ni dada yangu." Ambapo alikuwa. Kasema, "Wewe

sema u dada yangu." Kwa sababu, mnaona, katika siku hizo (Huenda nikaweka kizibo hapa kama mhubiri anataka kuhubiri juu yake wakati mwingine, huenda ukalichambua kote katika Biblia.) kumbukeni, wanaume walikuwa na wake wengi kadiri walivyoweza kuwa nao, lakini hakuna mwanamke angeweza kuwa na waume wawili walio hai kwa wakati mmoja. Daudi alikuwa na wake mia tano, lakini hakuna hata mmoja wao aliyekuwa na mume mwingine. Um-hum. Afadhali nikome, sasa hivi. Mnaona? Vema. Laiti wangalijua ukweli wa jambo hilo, ungeyararua makanisa haya waziwazi, hiyo ni kweli.

225 Sasa, angalieni kile kingetukia kama ungefikia tu ambapo Mungu angeweza kukufunulia mambo fulani ya Roho!

226 Sasa angalieni, sasa, yeye alisema, "Sasa, wataniua, na kukuokoa hai." Maana almuradi tu alikuwa amemwoa... Kasema, "Sema wewe ni dada yangu, na hilo litakuwa jema kwangu."

227 Sasa, huyu hapa Ibrahimu akishuka kwenda kule, na huyu hapa maskini Sara, maskini nyanya, mwajua, akija, ndipo Abimeleki akasema, "Loo, huyo hapo mrembo, huyo ndiye ninayemtaka, nyanya!"

228 La, hilo linasikika la kipumbavu, sivyo? Mnaona? Sivyo, yeye alikuwa ni mwanamke mrembo. Hakika, yeye ni kijana tena. Loo! Usijali, mama, siku moja inakuja, mwangalie baba, kuwa tu Uzao wa Ibrahimu, kuwa na imani hiyo, hiyo ndiyo inayohitajika. "Sisi tukiwa wafu katika Kristo, sisi ni Uzao wa Ibrahimu." Lakini inakubidi kuwa mfu katika Kristo, umvae Kristo, Roho Mtakatifu ndani yako, huo ni Uzao wa Ibrahimu, Naye atakufufua tena, uzee hautamaahisha kitu.

229 Nilimwuliza *sayansi*, hapa si muda mrefu uliopita, nikasema, "Naomba uniambie jambo fulani. Ati kila wakati ninapokula, nimeumbwa kwa mavumbi ya ardhi, na kila ninapokula chakula ndipo ninayafanya upya maisha yangu?"

Akasema, "Hiyo ni kweli. Hutengeneza mishipa ya damu, na—na damu, unapata damu mpya kutoka kwenye chakula chako," kisha kasema, "hiyo inafanya maisha mapya."

230 Nikasema, "Unajua, nilipokuwa na umri wa miaka kumi na sita, nilikula chakula kile kile ninachokula sasa," nami nikasema, "kila wakati nilipokula, nilikuwa mkubwa zaidi na mwenye nguvu zaidi, sasa haidhuru ninakula kiasi gani, ninaendelea kuzeeka na kudhoofika. Kama ninayafanya upya maisha yangu, yako wapi, yanapatwa na nini? Hebu niambie, nina jagi ya maji na bilauri ya ma-...zimewekwa hapa, nami ninaanza kumwaga maji kutoka kwenye jagi hili kubwa kuyamiminia kwenye hii bilauri, nayo inaanza kujaa, na kufikia nusu, nami ninaanza kumwagilia haraka zaidi, nayo yanaendelea kupungua wakati wote, nithibitishie hilo

kisayansi." Siwezi kueleza, naweza kwa Biblia, ni miadi. Hiyo ni kweli.

231 Hiyo ni kweli. Mungu amechagua, wakati alipokuona wewe na mama katika umri unaofaa, ulipokuwa kijana na umeoa na mwenye furaha, unakumbuka hilo, baba? Kabla watoto hawajazaliwa, muda si muda wajua, yeye ndiye kitu kizuri sana ulichowahi kuangalia. Loo, jamani, ulifikiri tu alikuwa ni mrembo; na jinsi alivyokupenda, ukisimama, hayo mabega yaliyonyoka.

Baada ya kitambo kidogo, ukaangalia kote, na kusema, "Mama, kuna makunyanzi yanayokuja chini ya macho hayo mazuri."

"Naam, Baba, mvi kidogo inakuja *hapa*, pia, ikienea juu."

232 Kuna nini? Unaona, mauti yameingia, yatakutia hatarini siku moja, lakini sikilizeni, katika ule ufufuo hakutakuwako na kitu kimoja kinachowakilisha mauti, tutakuwa wapya. Haleluya!

233 Nina yapata nywele nne ama tano zilizosalia juu, nami nilikuwa nikizichana siku chache zilizopita, ama wakati fulani uliopita, nikizichana, ndipo mke wangu akasema, "Billy, unajua nini? Karibu una upara, Mpenzi."

Nikasema, "Lakini sijapoteza hata mmoja wazo."

Akasema, "Naomba uniambie zilipo."

234 Nikasema, "Ngoja kidogo, Mpenzi, njoo hapa." Nikasema, "Hebu niambie, kab-. . .zilikuwa wapi kabla sijazipata, ilibidi zitoke mahali fulani, niambie zilikuwa wapi kabla sijazipata, nitakwambia zilipo, zikiningojea niziendee."

235 Haleluya! Mungu wangu ni Mungu wa Ibrahimu. Amina. Kila unywele wa kichwa chako umehesabiwa. Makunyanzi yote yatapita, uzee utapita. Loo, utukufu kwa Mungu! Nasi tutakuwa kiumbe kipya milele, tukisimama katika fahari ya ujana na furaha. Amina. Huyo ndiye Mungu wetu.

236 Loo, nitakuwa ninii, ninii tu, labda kijiko kimoja cha mavumbi, bali Yeye ataniita siku moja, niende, "*Fiu*! Njoo huku, Billy."

Niseme, "Mimi hapa, Bwana, mimi hapa, Baba." Naam, bwana.

Kamwe hatakuja aseme, "Sasa, Bw. Branham, Charles, wewe na Ella mzaeni William tena, maana alikuwa mmoja wa watumishi Wangu."

La, la. Yeye *atanena* tu, nami nitamjibu. Amina. Haleluya! *Haleluya* maana yake ni, "Mungu wetu asifiwe." Nafikiri Yeye anastahili sifa zote.

237 Mtu fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, akasema, mwanamke aliyekuwa mfuasi wa kanisa lingine la

kimadhehebu, akasema, "Ndugu Branham, kuna kasoro moja tu ya huduma yako ninayoona."

Nikasema, "Ni kitu gani hicho?"

Kasema, "Unamjivunia Yesu kupita kiasi."

Nikasema, "*Ati* ninafanya *nini*?"

Kasema, "Unamjivunia kupita kiasi, unamfanya Mungu."

Nikasema, "Yeye alikuwa ni Mungu."

Naye akasema, "Loo, alikuwa ni nabii."

Nikasema, "Yeye alikuwa ni zaidi ya nabii, Yeye alikuwa ni Mungu wa manabii." Hiyo ni kweli.

238 "Loo," akasema . . . Mnajua ninazungumzia dini gani, sitaki kuwaudhi, ilikuwa ni mwanamke wa Sayansi ya Ukristo. Mnaona, maana wengi wao huja mkutanoni, wanaponywa, hilo ni sawa. Akasema, "Vema, yeye alikuwa—alikuwa ni mtu mzuri, ninaamini alikuwa ni nabii."

Nikasema, "Ama alikuwa Mungu, au mdanganyifu mkubwa kuliko wote ulimwengu uliyepata kuwa naye." Alikuwa Mungu Mwenyewe.

Naye akasema, "Nitalithibitisha kwa Biblia yako mwenyewe, ulisema ulikuwa wa kimsingi, nitathibitisha kwa Biblia yako mwenyewe ya kwamba yeye hakuwa kitu ila mwanadamu."

Nikasema, "Hebu lithibitishe."

239 Naye akasema, "Yohana Mtakatifu mlango wa 11, wakati Yesu aliposhuka kwenda kwenye kaburi la Lazaro, Biblia ilisema alilia, hiyo ilithibitisha ya kwamba alikuwa ni mwanadamu, kama ulivyo wewe."

Nami nikasema, "Hayo ndiyo Maandiko yako?"

Akasema, "Ndiyo."

Nikasema, "Dada, hiyo ni nyembamba kuliko mchuzi uliotengenezwa kwa kivuli cha kuku aliyekufa kwa njaa." Nikasema, "Hiyo haitasimama kamwe."

Akasema, "Unamaanisha nini kwa hilo?"

240 Nikasema, "Alilia kama mwanadamu, hiyo ni kweli, akienda kaburini, lakini alipoyasimamisha mabega Yake madogo, yaliyoinama, na kuyavuta pamoja, na kusema, 'Lazaro, njoo huku,' na mtu aliyekuwa amekufa siku nne akasimama kwa miguu yake, akaishi tena, hiyo ilihitaji zaidi ya mwanadamu." Naam, bwana. Mungu!

241 "Mimi ndimi Ufufuo na Uzima," asema Mungu. Si mwanadamu, si nabii, bali Mungu, hivyo ndivyo alivyokuwa. "Mimi ndimi Ufufuo na Uzima," asema Mungu. "Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Kila aishiye

na kuniamini Mimi hatakufa kamwe." Kasema, "Je, unaamini jambo hili?"

Naye akasema, "Naam, Bwana, ninaamini." Jambo ndilo hilo, jambo fulani halina budi kutukia. Si mwanadamu, Mungu.

242 Sasa, hebu tumfuate Ibrahimu. Kwa hiyo, Sara, Abimeleki akasema, "Unajua, huyo hapo mwanamke mrembo wa Kiebrania." Kasema, "Huyo ni mume wako?"

"La, huyo ni ndugu yangu."

Mume akasema, "Hiyo ni kweli, huyo ni—huyo—huyo ni dada yangu." Ambapo alikuwa, dada yake wa kambo.

"Vema," kwa hiyo akasema, "vema, nitampeleka kwenye ikulu, nami . . . atakuwa mke wangu, nami nitakupa tu vitu vingi sana. Mnaona?"

"Vema."

Kwa hiyo akampeleka kule.

243 Nanyi mngeweza kuwazia mtu akifanya jambo kama hilo? Kwa hiyo, akaingia pale . . . Mnaona, kwa nini—kwa nini—ni kwa nini akafanya hivyo? Kwa nini alipatana? Alikuwa nje ya ile ahadi, alishuka akaenda Gerari.

244 Hiyo ndiyo sababu ninyi wanawake mnakata nywele zenu, na kutumia vipodozi, nanyi jamaa mnavuta sigara, na—na kuendelea jinsi mnavyofanya, mnatoka nje ya ahadi, na bado mngali mashemasi, na washiriki, na kadhalika, kama wafanyavyo hawa Wabaptisti, Wapresbiteri, Wamethodisti, Wapentekoste, na kadhalika, mnatoka tu moja kwa moja kwenye ahadi, hivyo tu, ibilisi aliwasukumia ninii yoyote . . . Kaeni hapa, mahali penu, mkiomba sana! Hiyo ni kweli, mnamwacha ibilisi aseme nanyi, mnamsikiliza.

245 Sasa, huyu hapa, ameketi huko nje kama maskini mwoga anayenyemelea. Ameketi nje . . . Mungu anisamehe kwa kunena juu ya nabii Wake namna hiyo, lakini ninajaribu kutoa hoja hapa.

246 Sasa, tunaangalia, maskini Abimeleki alienda kule, nami ninawazia usiku huo baada ya kuoga, na kuvaa pajama yake, na kukariri sala zake, na kunyoosha vidole vyake vya miguu namna *hiyo*, "Loo, hatimaye nimempata yule niliyemtaka. Hmm!" Akiwa amelala kitandani, kasema, "Kesho, nitamwoa mwanamke huyu mrembo, wa Kiebrania." Walikuwa wamempamba kabisa kwa hereni, na vitu vya namna hii vyote, mwajua. "Loo, jinsi anavyoonekana mrembo! Kesho, nitamwoa."

247 Ndipo alipokuwa amelala pale kitandani, Bwana akasema, "Wewe ni kama tu mtu aliyekufa." Huyo ndugu mwema, mtakatifu, bali Yeye alisema, "Wewe ni kama tu mtu aliyekufa." Kasema, "Mwanamke huyo ni mke wa mwanamume mwingine."

Vema, akasema, “Bwana, unajua unyofu wa moyo wangu. Hivi yeye hakuniambia hivyo?”

“Naam, najua.”

“Hivi hakuniambia?”

248 “Naam, najua, hiyo ndiyo sababu nilikuzuia usinitende dhambi. Sasa, mumewe ni nabii Wangu.” Amina. Sasa, kama unataka kuangalia neema, angalia jambo hili. Ameketi huko nje akidanganya kuhusu mkewe. “Lakini mumewe ni nabii Wangu. Sitasikia maombi yako, lakini mrudishe, na umwache akuombee, ndipo nitakuponya.”

249 Loo, haleluya! Loo, ndugu, unaweza kuliona? Uzao wa Ibrahimu ulitia nanga ndani ya Yesu! “Mumewe ni nabii Wangu.” Haya basi. “Mrudishie mke wake, na umpe sadaka, na umwache akuombee,” maana Yeye alifunga kila tumbo la uzazi. Hiyo ni kweli. Hilo taifa lingekufa papo hapo, wala lisingebaki tena.

250 Lakini alikuwa tayari, alikuwa mtu mwema, alienda akamchukua mke wake na kumrudisha, ndipo Mungu akambariki na kumbariki Ibrahimu. Ndipo akaanza kurudi kwenye nchi ya uenyeji wake, moja kwa moja akarudi mahali ambapo Malaika alikutana naye, na kumwonyesha ishara kwa kumpa kisogo. Mungu yuyo huyo anaishi usiku wa leo.

251 Sitakuwa na wakati wa kuendea hili lingine, nitalichukua kesho kwenye Shule ya Jumapili, tamshi hili dogo la mwisho hapa. Nina—nina wa 21, 20, sehemu ya mwisho ya mlango wa 20 na 21, hata hivyo, bado, pamoja na Maandiko fulani pale ningetaka kutumia. Nami nitayaendea hayo kesho kwenye Shule ya Jumapili, jinsi Yeye anavyomchukua na kuwa Yehova-yire.

252 Loo, ndugu, Malaika wa Bwana yuko—yuko hapa, usiku wa leo. Yeye ni Yehova Mungu katika mwili wako, Yeye ni Yehova Mungu katika mwili wangu, Mungu yuyo huyo hafi, Yeye ni halisi tu vivyo hivyo. Jambo ni kwamba, watu hawamtambui. Hawamta-. . . Naye ajapo, wao wanasema, “Vema, vema sana, nadhani. Inaonekana ni sawa, um-hum. Nadhani hiyo ni kweli.”

253 Loo, ndugu, kama kila Neno katika Biblia hiyo si la kweli, si Neno la Mungu, si Neno la Mungu endapo si kweli. Lakini kama ni kweli, basi ni—ni . . . kama ninii . . . Kama Mungu akilithibitisha Neno Lake, basi ni kweli. Amina. Mungu hutimiza Neno Lake, hivi hamwamini hilo?

254 Yupo hapa, Yupo hapa. Ninasema hilo katika Jina la Bwana. Unafikiri ndivyo alivyo? Sasa, Yeye anaweza kutumia mwili wangu kama vile angeweza kuumba mingine, maana Yeye aliniumba, kwa vyovyote vile. Yeye angeweza kutumia mwili wako, alikuumba, akakufanya, hivi huoni hivyo? Sasa, kama utaufungua tu moyo wako, na kujiondoa njiani, Yeye ataingia, anaweza kukutumia. Yeye ni Mungu yeye yule, anatoa

ishara zile zile. Amina. Unaamini hilo? Mwangalie Yeye, hebu nigeuze mgongo wangu, ombea shida fulani uliyo nayo. Loo, ni changamoto.

255 Naam, bwana. Huyu hapa mwanaume mbele yangu, huyu hapa amesimama moja kwa moja...Hebu nione sasa, yuko wapi? Ameketi moja kwa moja kule nyuma, tai imefunguliwa hapa mbele, amevaa suti nyepesi, nywele nyembamba juu, anaugua ugonjwa wa moyo. Huyo mtu aliyevaa suti ya kijivu, aliyeketi hapa akiniangalia moja kwa moja, ulikuwa ukiomba, "Bwana, jalia aniguse." Hiyo ni kweli? Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Kwamba Malaika yuyo huyo alikuja, akaniambia alichokuwa akisema moyoni mwake, basi kwa nini si Mungu yeye yule? Ugonjwa wako wa moyo umekwisha, Ndugu, nenda nyumbani ukawe mzima. Amina. Isingewezekana uwe na kadi ya maombi, sivyo? Huna kadi ya maombi, huhitaji moja.

256 Mnaona ninalomaanisha? Ninii...Mnaona, anajirudia tu. Niliangalia kote, nikamwona amesimama kule nyuma, hizo nywele nyembamba, nikaangalia, nikawaza, "Yuko wapi?" Nikaangalia huko nyuma na huyo hapo, alikuwa ameketi pale. Huyo mtu, ninii tu, sijawahi kumwona maishani mwangu.

Kama hatufahamiani, inua mkono wako, bwana. Kila neno lililosemwa, ni kweli? Je, hivyo ndivyo ulivyokuwa ukiwazia, ulichokuwa ukifanya? Haya basi.

257 Basi Yeye alisema nini? Wakati huyo, Mtu huyo aliyeketi hapo, Mungu katika mwili Wake, mwili wa Mtu huyu, kasema, "Kwa nini Sara akasema moyoni mwake, ya kwamba haiwezekani?" Ndipo Malaika yuyo huyo akaja hapa. Na akasema, "Kwa nini...? Ulisema itatendeka, jalia aniguse." Amina.

258 Loo, kwa nini mwe wazito hivi? Amina. Iweni tu na imani. Hivi hamwoni, enyi marafiki? Mwaweza kuamka, enyi Wapentekoste? Kwa nini usiume dhamiri yako? Kwa nini usiifinye nafsi yako?

Amina. Sasa, inaanza kila mahali. Loo, Yehova-yire, Bwana anaweza kujitolea Mwenyewe dhabihu. Amina. Iweni na imani.

259 Unawazia nini, Ndugu? Nadhani huenda mkafikiri mimi ni mkali, sivyo nilivyo. Mimi ni ndugu yenu, mimi ni ndugu yenu. Hiyo ni kweli, Ndugu, ninawapenda. Ninatambua niko katika ka—kanisa la kimadhehebu hapa, Assembly of God, mojawapo wa wadhamini wangu wakuu sana, ndugu zangu. Lakini ninachochukia kuona ni kuingia baridi na kupoa. Sipingi dhehebu hilo, siwapingi ndugu wa Umoja huko nje, ama Wamethodisti, ama Wabaptisti, ninasema jambo lilo hilo kila mahali, ila kile ninachojaribu kusema, "Jitikiseni, ndugu. Yaondoeni macho yenu kwenye mambo haya."

260 Hapa, ngoja kidogo, mwanamke mmoja alitokea hapa mbele yangu, mtu fulani akiomba, ugonjwa wa neva, macho. Huyo

mwanamke amevaa nguo nyekundu. Huyu hapa ameketi papa hapa. Unaamini ya kwamba Yeye atakuponya? Bibi Curry, basi kama utaamini kwa moyo wako wote, Mungu atakuponya. Hiyo ni kweli, inua mkono wako. Vema, haya basi.

261 Ninakupa changamoto kuamini. Ni kitu gani? Bwana Mungu Mwenyezi yule yule, yuko hapa ndani, akiishi katika mwili wa mwanadamu. Haleluya! Haleluya! Loo, jamani! Roho Yake iko kote jengoni.

262 Yule mwanamke aliyenena naye alikuwa wapi? Yuko wapi? Ni, ilikuwa ni wewe, mama? Yule mwanamke aliyenena naye wakati huo, alikuwa wapi? Loo, hapa, mama huyu, naam. Vema. Unakubali uponyaji wako sasa? Sikujui, sijawahi kukuona maishani mwangu, sijui lolote kukuhusu, lakini mambo hayo ni kweli, sivyo?

Haya basi. Vema. Vema. Mnaona, sijawahi kumwona, hiyo hapo mikono yangu mbele za Mungu. Mnaona yale Yeye afanyayo?

263 Loo, ndugu, dada, kama ungeondoka tu kwenye ganda lako, ujiondoe kwalo! Toka, ujiweke mbele za Mungu, huku ukisema, “Bwana Mungu, sileti chochote mikononi mwangu, ninaushikilia tu msalaba Wako.” Hiyo ni kweli.

Nitamsifu, nitamsifu,
Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa ajili ya wenye dhambi;
Mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha na kuondolea mbali kila doa.

Nitamsifu, nitamsifu,
Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa ajili ya wenye dhambi;
Mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha na kuondolea mbali kila doa.

Nampenda, na-. . .

Loo, jamani, mwabuduni. Hayo mahubiri magumu, makali yamekwisha sasa, hebu tumwabudu Yeye.

. . .Alinipenda kwanza (Hivi humpendi? Yeye si ni wa ajabu?)
. . .kununua . . .wokovu
Mtini Kalvari.

Nitamsifu, (Hivi hujisikii umesuguliwa kabisa sasa?) Nitamsifu,
Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa ajili ya wenye dhambi;
Loo, mpeni utukufu enyi watu wote,

Kwa kuwa Damu Yake imeosha na kuondolea
mbali kila doa.

264 Loo, hilo si linakufanyia jambo fulani? Roho ya kukata akipitia jengoni akikatakata, akitahiri. Neno *kutahiri* linamaanisha nini? "Kukatilia mbali nyama ya ziada." Kanisa lina nyama nyingi kupita kiasi za ziada, Upanga wa Mungu unazikata, ndipo tunapofanya hivyo, tunajisikia tumetahiriwa kabisa na ni safi. Paulo alisema, "Ninamwabudu Yeye, ninamwabudu katika Roho."

Nitamsifu, nitamsifu,
Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
ajili ya wenye dhambi;
Mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha na kuondolea
mbali kila doa.

265 Loo, Yeye si ni wa ajabu? Kuna mwenye dhambi hapa anayejua ya kwamba Mungu hufanya ahadi, Mungu hutimiza ahadi Yake? Mungu anazungumza hapa, na kukiwepo mtu anayehubiri Neno la Mungu, Mungu ataliunga mkono Neno Lake. Sasa, si lazima ubahatishe kulihusu, Yeye yu hai, Yeye yupo hapa sasa. Je, unamtaka kama Mwokozi wako? Njoo madhabahuni kama unamtaka, tunapoimba tena. "Nitamsifu, msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa ajili ya wenye dhambi." Vema. Utakuja madhabahuni?

Nitamsifu, nitamsifu,
Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
ajili ya wenye dhambi;
Mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha na kuondolea
mbali kila doa.

266 Loo, ajabu! Ingekuwaje huko India kama wito huo wa madhabahuni ungefanywa namna hiyo? Ingekubidi kurudi, wangekusongamania mno, yapata maelfu wakimiminika madhabahuni, wanampenda, wanapomwona Mungu, si nyenzo, si Mungu ambaye ni Mungu wa kihistoria, Mungu ambaye ni Mungu wa leo hii.

267 Mungu kutoka kwenye historia hujifanya Mwenyewe. . . Nitakuwa nikihubiri juma hili lijalo: *Mungu Wa Historia Akijitokeza Jukwaani*. Angalieni kama Yeye ni Mungu wa kihistoria, ama kama Yeye si Mungu yeye yule, leo. Amina. Ninampenda, nanyi je?

Imani yangu inakutegemea Wewe,
Ewe Mwana-Kondoo wa Kalvari,
Mwokozi wa Kiungu;
Sasa nisikie ninapoomba,
Ondolea mbali dhambi zangu zote,
Ee nijalie tangu leo

Kuwa Wako kabisa!

Huku nikikanyaga kwenye mzingile wa maisha
wenye giza,
Na huzuni zimenizunguka,
Uwe Kiongozi wangu;
Agiza giza ligeuke kuwa mchana,
Futilia mbali machozi ya huzuni,
Wala usiniache nipotee kamwe
Kutoka Kwako kwenda kando.

Hivi mtu mwingine si aje madhabahuni wakati hawa wakiwa hapa, nafsi zilizotubu zikilia?

Imani yangu inakutegemea Wewe,
Ewe Mwana-Kondoo wa . . .

Njoo, rafiki mwenye dhambi, kamwe hutakuwa karibu zaidi.

Mwokozi wa Kiungu;

Vipi kuhusu Mkristo vuguvugu? Kwa nini usije huku, ukaombe vya kutosha?

Sasa, nisikie ninapoomba,
Ondolea mbali dhambi zangu zote,
Wala usiniache nipotee kamwe
Kutoka Kwako kwenda kando.

268 Hivi hutakuja? Njoo msalabani kwa utamu, kwa unyenyekevu. Mungu awabariki, wale wanaokuja. Shuka moja kwa moja na uingie sasa, karibu na madhabahu. Hebu na tuwe na msimu wa maombi. Kwa nini si wale mnaojisikia unyevu kidogo rohoni mwako? Njoo, Dada mpendwa, ninakuona moja kwa moja kwenye roshani ukija, njoo.

Vile tu nilivyo, bila hata ombi moja,
Lakini kwamba Damu Yako ilimwagwa kwa
ajili yangu,
Kwa sababu Wewe uliahidi, naamini,
Ee Mwana-Kondoo wa Mungu, naja!

Jambo ndilo hilo. Sasa ubaridi utaanza kuvunjika.

Vile tu nilivyo, bila hata ombi moja,
Lakini kwamba Damu Yako ilimwagwa kwa
ajili yangu,
Kwa sababu ninaahidi . . . naja Kwako,
Ee Mwana-Kondoo wa Mungu, naja! Naja!

Vile tu nilivyo, wala singojei
Kuondoa doa moja jeusi nafsini mwangu,
Kwako Wewe, ambaye Damu Yako inaweza
kusafisha kila doa,
Ee Mwana-Kondoo wa Mungu, naja! Naja!

269 Sasa, kila mmoja wenu, inamisheni vichwa vyenu, mwinulieni Mungu mikono yenu, na mwanze kuomba, omba

mwenyewe. Shuka moja kwa moja uanze kuomba. Ndivyo hivyo . . . ? . . .

61-0211 Ibrahimu
First Assembly Of God Of Long Beach
Long Beach, California Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org